
# Elimu ya Dini ya Kiislamu

## Shule za Sekondari

## Kitabu cha 1



Islamic Education Panel

# Neno la Awali

Vitabu vya somo la “Elimu ya Dini ya Kiislamu(Islamic Knowledge O’Level) ” kwa ajili ya Wanafunzi wa shule za Sekondari, vimekuwa ni hitajio kubwa la muda mrefu kwa kuzingatia hitajio hili, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikishirikiana na Baraza Kuu la Waislamu wa Tanzania,imechukukua jukumu la kuandaa Vitabu vya “Elimu ya Dini ya Kiislamu kwa shule za Sekondari kwa kufuata muhtasari wa kila kidato. Pana mfululizo wa vitabu vinne kwa ajili ya kidato cha kwanza hadi cha nne.

Kama ilivyo katika muhtasari, somo la Elimu ya dini yaKiislamu(Islamic Knowledge O'Level) limegawanywa katika fani zifuatazo:

(i) Tawhiid
(ii) Fiqh
(iii) Qur'an
(iv) Sunnah na Hadith
(v) Historia ya Kiislamu(Tarekh)

Kwa urahisi wa kupata mtiririko unaokwenda sambamba na fani hizi, Vitabu vyote vinee vya somo hili vimegawanywa katika Sura zinazolanda na fani hizi. Kila mwanzo wa sura kuna utangulizi unaoonyesha mada zitakazofundishwa kulingana na muhtasari wa kidato kinachohusika.

Tunamshukuru Allah(s.w) kwa kutuwezesha kutoa kitabu hiki cha kwanza. Ni tumaini letu kuwa wanafunzi na waalimu wanaofundisha
somno hili watafaidika vya kutosha waalimu wanaofundisha somo hili watafaidika vya kutosha. Pia vitabu hivi vitawasaidia waislamu na wasiokuwa Waislamu wenye nia na ari ya kutaka kuujua Uislamu.

Mwanafunzi wa Kiislamu au Muislamu yeyote baada ya kuyapitia mafunzo ya kitabu hiki na kuyafahamu vilivyo, hana budi kuyaingiza katika matendo na kuwa na mwenendo unaolingana na mafunzo hayo ili aweze kupata radhi za Allah(s.w). K utenda kinyume na ujuzi wa yakini ulioupata ni katika mambo yanayomchukiza sana Allah(s.w) kama anavyotuasa:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ لِمَ تَقُولُونَ مَا لَا تَفۡعَلُونَ ٢

كَبُرَ مَقۡتًا عِندَ ٱللَّهِ أَن تَقُولُواْ مَا لَا تَفۡعَلُونَ ٣

*“Enyi mliamini! Mbona mnasema msiyoyatenda? Ni chukizo kubwa mbele ya Allah kusema msiyoyatenda”(61:2-3)*

Tunatoa wito kwa wasomaji wote wa kitabu hiki cha kwanza kutoa maoni yao na mapendekezo ili kuborehsa mafunzo haya kwa walengwa na kufikia lengo lililokusudiwa. Maoni na mapendekezo yanayofaa yatazingatiwa katika chapisho la pili.

# *Sura ya Kwanza*

# TAWHIID

Katika kitabu hiki somo la Tawhiid litajihusisha na mada kuu zifuatazo:

- Maana ya Tawhiid na Aina zake
- Mtazamo wa Uislamu Juu ya Elimu
- Mtazamo wa Uislamu Juu ya Dini
- Imani ya Kiislamu

# MAANA YA TAWHIID NA AINA ZAKE

**Maana ya Tawhiid**

- Neno Tawhiid ni unganisho (kufanya kitu kuwa kimoja) na linatokana na neno la kiarabu '*Wahhada', lenye maana ya kuunganisha kufanya kitu* kimoja.
- Lakini neno Tawhiid linapotumika kumuelezea Mwenyezi Mungu (yaani Tawhiidullah) lina maana ya "*Kumpwekesha Mwenyezi Mungu*" katika kila kitu, kwamba yeye ni Mmoja na Umoja wake unatosha kwa kila kitu na kila jambo na hana mshirika.

- Kwa muktadha huo, Tawhiid basi ni Imani kuwa Mwenyezi Mungu ni Mmoja, hana mshirika katika Utawala na matendo yake; hana mfano katika asili yake wala sifa zake; wala hana mpinzani katika Uungu wake na kuabudiwa kwake.
- Kwa hakika Tawhiid ni dhana ya kimapinduzi inayolenga kumkomboa mwanaadamu kutoka katika giza la ujahili na ukafiri kumpeleka kwenye mwanga,kutoka katika utumwa kwa mwanadamu na kuwa mtumwa kamili wa Allah(s.w).
- Kutokana na maelezo haya ndio tunapata mafungu makuu matatu ya Tawhiid ambayo:

# Aina Kuu za Tawhiid

1. Tawhiid – Rubbuubiyya (yaani, kumpwekesha Mwenyezi Mungu katika Utawala wake).
2. Tawhiid – Asmaa wassifaat (yaani, Kumpwekesha Mwenyezi Mungu katika majina na sifa zake).
3. Tawhiid – Ibaadah (yaani, Kumpwekesha Mwenyezi Mungu katika kuabudiwa).

- Vipengele hivi vitatu ndivyo vinavyofanya msingi wa sayansi ya Tawhiid.
- Vyote vitatu vinategemeana, na kuacha kimojawapo kunaitia dosari Imani nzima ya Tawhiid.
- Kipengele kimoja tu katika hivyo kikikiukwa basi mtu huzama kwenye Shirk, ambayo ina maana ya kumshirikisha mwenyezi mungu, na huko humtoa mtu katika Uislamu.

# MTAZAMO WA UISLAMU JUU YA ELIMU

## Maana ya elimu

- Elimu ni ujuzi ulioambatanishwa na utendaji.
- Wanataaluma wamejitahidi kutoa maana ya elimu kuwa ni mabadiliko ya tabia yanayotokana na ujuzi.
- Kwa maana hii Elimu haiishii kwenye kuijua tu bali elimu hukamilika inapomwezesha mwenye kujua kutenda kwa ufanisi zaidi kuliko yule asiyejua.

**Nani aliye elimika?**

- Kutokana na maana ya elimu tuliyojifunza hapo juu, mtu aliyeelimika ni yule ambaye ujuzi alioupata humuwezesha kutenda kwa ufanisi zaidi kuliko pale alipokuwa hajapata ujuzi huo.
- Mtu aliyesoma hatachukuliwa tu kwa kirahisi kuwa kaelimika, bali kuelimika au kutoelimika kwake kutathibitika katika matendo na mwenendo wake wa kila siku.

- Matarajio ni kwamba mtu aliyesoma anapaswa aelimike kwa kutenda kwa ufanisi zaidi kuliko asiyesoma.
- Ni katika kuzingatia hili Allah(s.w) anatukumbusha katika Qur-an:

…………… قُلْ هَلْ يَسْتَوِى ٱلَّذِينَ يَعْلَمُونَ وَٱلَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ ۗ إِنَّمَا يَتَذَكَّرُ أُو۟لُوا۟ ٱلْأَلْبَٰبِ ۝٩

*“…………Sema, Je, wanaweza kuwa sawa wale wanaojua na wale*
*wasiojua? Wanaotanabahi ni wale wenye akili tu.” (39:9)*

- Jibu la swali hili ni wazi.
- Mjuzi na asiyejua hawawezi kuwa sawa kiutendaji na kitabia.
- Endapo mtu atajiita msomi kwa kusoma vitabu vingi au kupewa shahada nyingi lakini kitabia na kiutendaji akawa hatofautiani na wale wasiosoma atakuwa bado hajaelimika na mfano wake ni ule unaopigwa katika Qur-an:

مَثَلُ ٱلَّذِينَ حُمِّلُوا۟ ٱلتَّوْرَىٰةَ ثُمَّ لَمْ يَحْمِلُوهَا كَمَثَلِ ٱلْحِمَارِ يَحْمِلُ أَسْفَارًۢا ۚ بِئْسَ مَثَلُ ٱلْقَوْمِ ٱلَّذِينَ كَذَّبُوا۟ بِـَٔايَـٰتِ ٱللَّهِ ۚ وَٱللَّهُ لَا يَهْدِى ٱلْقَوْمَ ٱلظَّـٰلِمِينَ ﴿٥﴾

*"Mfano wa wale waliopewa Taurati kisha hawakuichukua (kwa kuitia katika matendo) ni kama punda aliyebeba (mzigo) wa vitabu vikubwa (bila ya kufaidika kwavyo) ni mbaya kabisa mfano wa watu waliokadhibisha aya za Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu madhalimu." (62:5).*

# Nafasi ya Elimu na wenye Elimu katika Uislamu

Nafasi ya elimu na mwenye elimu katika uislamu inaonekana katika maeneo yafuatayo:

➢ **Kwanza, Elimu ndio takrima ya kwanza aliyokirimiwa mwanaadamu** na Mola wake.Tunajifunza katika Qur-an kuwa jambo la kwanza alilotunukiwa Adam (a.s) mara tu baada ya kuumbwa kwake ni kupewa elimu.

وَعَلَّمَ ءَادَمَ ٱلْأَسْمَآءَ كُلَّهَا

*"Na Mwenyezi Mungu akamfundisha Adam majina ya vitu vyote..." (2:31)*

*“Majina ya vitu vyote” katika aya hii inaashiria fani zote za elimu* ambazo anahitajia mwanaadamu hapa duniani ili afikie kwa ufanisi lengo la kuumbwa kwake.

Pia tunajifunza katika Quran kuwa mwenye elimu na hekima amepewa kheri nyingi.

يُؤْتِى ٱلْحِكْمَةَ مَن يَشَآءُ ۚ وَمَن يُؤْتَ ٱلْحِكْمَةَ فَقَدْ أُوتِىَ خَيْرًا

كَثِيرًا ۗ وَمَا يَذَّكَّرُ إِلَّآ أُو۟لُوا۟ ٱلْأَلْبَٰبِ ﴿٢٦٩﴾

*(Mwenyezi Mungu ) humpa hikma amtakaye, na aliyepewa hikma bila shaka amepewa kheri nyingi. Na hawakumbuki ila wenye akili. (2:269).*

Kutafuta elimu (kusoma) ni amri ya kwanza kwa mwanaadamu. Tunajifunza kutokana na historia ya kushushwa Qur-an kuwa Wahay wa kwanza kumshukia Mtume (s.a.w) ambao ndio ulimtawazisha rasmi kuwa mtume ni ule unaopatikana katika aya tano za mwanzo za Suratul-A'laq:

ٱقۡرَأۡ بِٱسۡمِ رَبِّكَ ٱلَّذِى خَلَقَ ١ خَلَقَ ٱلۡإِنسَٰنَ مِنۡ عَلَقٍ ٢ ٱقۡرَأۡ وَرَبُّكَ
ٱلۡأَكۡرَمُ ٣ ٱلَّذِى عَلَّمَ بِٱلۡقَلَمِ ٤ عَلَّمَ ٱلۡإِنسَٰنَ مَا لَمۡ يَعۡلَمۡ ٥

*“Soma kwa jina la Mola wako aliyeumba.Ambaye amemuumba mwanaadamu kwa A’laq (pande la damu). Soma na Mola wako ni karimu sana. Ambaye amemfundisha mwanaadamu kwa kalamu. Amemfundisha mwanaadamu (chungu ya) mambo aliyokuwa hayajui”.(96:1-5)*

Kutokana na aya hizi, kwa muhtasari, tunajifunza yafuatayo:

1. Kusoma kwa ajili ya Mwenyezi Mungu ni jambo la kwanza waliloamrishwa wanaadamu na Mola wao.
2. Kusoma kwa jina la Mola wako ni kusoma kwa ajili ya kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu au ili kuweza kumwabudu Allah(s.w) inavyostahiki na kusimamisha Uislamu katika jamii.

3. Radhi za Mwenyezi Mungu zitapatikana pale mwanaadamu atakapoweza kufikia lengo la maisha yake, ambalo ni kumuabudu Allah(s.w) kwa kuzingatia maamrisho na mipaka ya Mwenyezi Mungu katika kukiendea kila kipengele cha maisha.

4. Amri hii ya kusoma hailengi fani maalum tu ya elimu; bali kila fani itakayomuwezesha mwanaadamu kufikia lengo la maisha yake kwa ufanisi.

5. Chanzo au chimbuko la fani zote za elimu ni Allah(s.w). Hivyo kwa Muislamu mlango wa kwanza wa elimu ni kusoma kwa mazingatio Qur-an na hadithi sahihi za Mtume(s.a.w) na kusoma Maarifa ya Uislamu kwa ujumla kutokana na vyanzo hivi viwili.

6. Hakuna mgawanyo wa Elimu Dunia na Elimu Akhera katika Uislamu

# Kwanini Uislamu umeipa Elimu nafasi ya kwanza?

Elimu imepewa nafasi ya kwanza katika Uislam kwa sababu zifuatazo:
**Kwanza, elimu ndio nyenzo pekee inayomuwezesha mwanaadamu** kumtambua Mola wake vilivyo na kumuabudu ipasavyo kwa unyenyekevu kama Qur-an inavyothibitisha:

إِنَّمَا يَخْشَى ٱللَّهَ مِنْ عِبَادِهِ ٱلْعُلَمَٰٓؤُا۟ ۗ

*“ Kwa hakika wanaomuogopa Mwenyezi Mungu miongoni mwa waja wake ni wale wataalam (waliozama katika fani mbali mbali)” (35:28).*

**Pili, elimu iliyosomwa kwa mrengo wa Qur-an ndio nyenzo pekee** inayomuwezesha mwanaadamu kuwa Khalifa wa Allah(s.w) hapa Ulimwenguni.

- Khalifa ni mja anayetawala ulimwengu kwa niaba ya Allah(s.w) kwa kufuata kanuni na sheria zake.
- Nabii Adam(a.s) aliwathibitishia Malaika kuwa ana uwezo wa kuutawala ulimwengu kwa niaba ya Allah(s.w) baada ya kuelimishwa fani zote za elimu (majina ya vitu vyote) na kuahidiwa mwongozo kutoka kwa Allah(s.w).

**Tatu, kutafuta elimu ni Ibada maalumu ya hali ya juu kuliko Ibada** zote. Kwa mujibu wa Qur-an Swala ni Ibada maalumu ya hali ya juu na ni dhikri kubwa au zingatio kubwa juu ya Allah(s.w)

................... إِنَّ ٱلصَّلَوٰةَ تَنۡهَىٰ عَنِ ٱلۡفَحۡشَآءِ وَٱلۡمُنكَرِۗ

وَلَذِكۡرُ ٱللَّهِ أَكۡبَرُ.................

*"Hakika swala humzuilia (mja) na mambo machafu na maovu na ni dhikri kubwa kwa Allah (s.w)." (29:45).*

Pia katika Hadith Mtume(s.a.w) amesisitiza:

*“Swala ndio nguzo kubwa ya Dini (Uislamu), mwenye kusimamamisha swala kasimamamisha Dini na mwenye kuacha swala kavunja Dini.”*

- Hivyo kwa mujibu wa Qur-an na Hadith sahihi za Mtume(s.a.w), swala ni Ibada yenye hadhi ya juu kuliko Ibada zote mbele ya Allah(s.w); lakini bado Ibada ya kutafuta elimu inachukuwa nafasi ya juu zaidi kuliko swala kwani swala haiwezi kusimama bila ya kuwa na ujuzi stahiki.

**Nne, mwenye elimu ana nafasi bora ya kumuabudu Mola wake** inavyostahiki katika kila kipengele cha maisha yake kama inavyosisitizwa katika Qur-an:

إِنَّمَا يَخْشَى ٱللَّهَ مِنْ عِبَادِهِ ٱلْعُلَمَٰٓؤُا۟ ۗ

*"Kwa hakika wanaomuogopa Mwenyezi Mungu miongoni mwa waja wake ni wale wataalamu." (35:28)*

Pia Qur-an inasisitiza juu ya umuhimu wa elimu kwa kuuliza:

……………. قُلْ هَلْ يَسْتَوِى ٱلَّذِينَ يَعْلَمُونَ وَٱلَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ ۗ

إِنَّمَا يَتَذَكَّرُ أُوْلُوا۟ ٱلْأَلْبَٰبِ ﴿٩﴾

*"……………..Je, wanaweza kuwa sawa wale wanaojua na wale wasiojua? Wanaotanabahi ni wale wenye akili tu." (39:9)*

Kimsingi wanaojua wanatarajiwa wafanye mambo kwa ufanisi zaidi kuliko wasiojua. Kwa msingi huu Allah(s.w) anasisitiza tena katika aya ifuatayo:

.............. يَرْفَعِ ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ مِنكُمْ وَٱلَّذِينَ أُوتُوا۟ ٱلْعِلْمَ دَرَجَٰتٍ..............

*"Mwenyezi Mungu atawainua (daraja) wale walioamini miongoni mwenu, na waliopewa elimu watapata daraja zaidi ."(58:11)*

- Hivyo, kutokana na aya hizi (35:28, 39:9 na 58:11) tunajifunza kuwa waumini wenye elimu wanadaraja zaidi kuliko waumini wengine kwa sababu wanao uwezo zaidi wa kuona dalili za kuwepo Allah(s.w) na utukufu wake kwa undani zaidi, jambo ambalo huwapelekea kumuogopa Mola wao na kumuabudu inavyostahiki katika kukiendea kila kipengele cha maisha yao kama inavyobainika katika aya zifuatazo:

إِنَّ فِي خَلْقِ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ وَٱخْتِلَٰفِ ٱلَّيْلِ وَٱلنَّهَارِ

لَأَيَٰتٍ لِّأُو۟لِى ٱلْأَلْبَٰبِ ﴿١٩٠﴾

*“Katika kuumbwa mbingu na ardhi na mfuatano wa usiku na mchana, ziko hoja (za kuonesha kuwepo Allah(s.w) kwa wenye akili. (3:190)*

ٱلَّذِينَ يَذْكُرُونَ ٱللَّهَ قِيَـٰمًا وَقُعُودًا وَعَلَىٰ جُنُوبِهِمْ وَيَتَفَكَّرُونَ فِى
خَلْقِ ٱلسَّمَـٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ رَبَّنَا مَا خَلَقْتَ هَـٰذَا بَـٰطِلًا سُبْحَـٰنَكَ
فَقِنَا عَذَابَ ٱلنَّارِ ١٩١

*“Ambao humkumbuka Mwenyezi Mungu wakiwa wima, wakiwa wamekaa na wakiwa wamelala. Na hufikiri (tena) umbo la mbingu na ardhi (wakasema) Mola wetu! Hukuviumba hivi bure bure tu. Utukufu ni wako. Basi tuepushe na adhabu ya moto.” (3:191).*

- Pia kutokana na aya hizo tunajifunza kuwa waumini wenye elimu wanaouwezo mkubwa wa kufanya mambo kwa ufanisi jambo litakalowapelekea kusimamisha ukhalifa wa Allah(s.w) katika jamii.

# Chanzo cha Elimu ni Allah(s.w)

Kama tunavyojifunza katika surat A’laq (96:4-5), chanzo cha elimu au mkufunzi wa binadamu ni Allah (s.w). Allah(s.w) huwasiliana na binadamu na kuwaelimisha kwa kutumia mojawapo ya njia zifuatazo zilizoainishwa katika aya ifuatayo:

۞ وَمَا كَانَ لِبَشَرٍ أَن يُكَلِّمَهُ ٱللَّهُ إِلَّا وَحْيًا أَوْ مِن وَرَآيِٕ حِجَابٍ أَوْ يُرْسِلَ
رَسُولاً فَيُوحِيَ بِإِذْنِهِۦ مَا يَشَآءُ ۚ إِنَّهُۥ عَلِيٌّ حَكِيمٌ ﴿٥١﴾

*“Na haikuwa kwa mtu kwamba Mwenyezi Mungu anasema naye ila kwa* ***il-hamu (anayetiwa moyoni mwake) au kwa nyuma ya pazia au humtuma mjumbe (Malaika) naye humfunulia kiasi anachotaka*** *kwa idhini yake (Allah), bila shaka yeye ndiye aliye juu mwenye hekima.” (42:51).*

Aya hii inatufahamisha kuwa binaadamu hupata habari kutoka kwa Allah(s.w) kwa njia tatu zifuatazo:

(a) Il-hamu.

(b) Kuongea na Allah(s.w)nyuma ya pazia.

(c) Kutumwa Malaika na kufikisha ujumbe kama alivyotumwa.

- Pia katika Qur-an tunafahamishwa njia mbili nyingine anazozitumia Allah(s.w) katika kumfikishia binaadamu ujumbe kutoka kwake:

(d) Ndoto za kweli (ndoto za Mitume).

(e) Maandishi (mbao zilizoandikwa tayari).

# (a) Il-hamu.

- Ni mtiririko wa habari au ujumbe unaomjia mwanaadamu bila ya kufundishwa na mtu yeyote au kuona mfano wake katika mazingira yoyote. Mambo mengi mwanaadamu huyafahamu kwa Il-hamu. Waasisi wa fani mbali mbali za elimu kama vile Hisabati, Fizikia, Jiografia, n.k.

Na Wavumbuzi wa vitu mbali mbali katika taaluma mbali mbali za kisayansi wameweza kufanya hivyo kwa kupata Il-hamu kutoka kwa Allah. Hivyo hakuna fani yoyote ya elimu isiyotoka kwa Allah (s.w).

عَلَّمَ ٱلْإِنسَٰنَ مَا لَمْ يَعْلَمْ ۝

*“Amemfundisha mwaanadamu mambo yote aliyokuwa hayajui” (96:5).*

## (b) Kuongea na Allah(s.w) nyuma ya Pazia

- Hii ni njia ambayo mwanaadamu huongeleshwa moja kwa moja na Allah(s.w) kwa sauti ya kawaida pasina kumuona.
- Kutokana na ushahidi wa Qur-an njia hii imetumika kwa Mitume na wateule wengine wa Allah (s.w).
- Nabii Mussa (a.s) ni miongoni mwa Mitume waliosemeshwa na Allah(s.w).kama tunavyofahamishwa kisa chake katika Qur-an:

۞ فَلَمَّا قَضَىٰ مُوسَى ٱلۡأَجَلَ وَسَارَ بِأَهۡلِهِۦٓ ءَانَسَ مِن جَانِبِ ٱلطُّورِ نَارٗاۖ قَالَ لِأَهۡلِهِ ٱمۡكُثُوٓاْ إِنِّيٓ ءَانَسۡتُ نَارٗا لَّعَلِّيٓ ءَاتِيكُم مِّنۡهَا بِخَبَرٍ أَوۡ جَذۡوَةٖ مِّنَ ٱلنَّارِ لَعَلَّكُمۡ تَصۡطَلُونَ ٢٩

*“Basi Musa alipotimiza muda, akasafiri pamoja na ahali zake (watu wake kurejea kwao Misri). Aliona moto upande wa mlimani akawaambia ahali zake; ‘Ngojeni, hakika nimeona moto, labda nitakuleteeni habari za huko au kijinga cha moto ili muote!”. (28:29)*

فَلَمَّآ أَتَىٰهَا نُودِيَ مِن شَٰطِيِٕ ٱلْوَادِ ٱلْأَيْمَنِ فِي ٱلْبُقْعَةِ ٱلْمُبَٰرَكَةِ مِنَ

ٱلشَّجَرَةِ أَن يَٰمُوسَىٰٓ إِنِّيٓ أَنَا ٱللَّهُ رَبُّ ٱلْعَٰلَمِينَ ﴿٣٠﴾

*“Basi alipoufikia aliitwa kutoka upande wa kuliani wa bonde hilo katika kiwanja kilichobarikiwa, kutoka mtini: “Ewe Mussa! Bila shaka mimi ndiye Mwenyezi Mungu, Mola wa walimwengu.” (28:30)*

- Kwa njia ya nyuma ya pazia, Nabii Mussa(a.s) aliongea na Allah mara nyingi na mara zote hizo hakuweza kumuona.
- Alipoomba amuone alijibiwa kama inavyoonyeshwa katika aya zifuatazo:

وَلَمَّا جَآءَ مُوسَىٰ لِمِيقَٰتِنَا وَكَلَّمَهُۥ رَبُّهُۥ قَالَ رَبِّ أَرِنِىٓ أَنظُرْ إِلَيْكَ ۚ قَالَ
لَن تَرَىٰنِى وَلَٰكِنِ ٱنظُرْ إِلَى ٱلْجَبَلِ فَإِنِ ٱسْتَقَرَّ مَكَانَهُۥ فَسَوْفَ تَرَىٰنِى ۚ
فَلَمَّا تَجَلَّىٰ رَبُّهُۥ لِلْجَبَلِ جَعَلَهُۥ دَكًّا وَخَرَّ مُوسَىٰ صَعِقًا ۚ فَلَمَّآ أَفَاقَ قَالَ
سُبْحَٰنَكَ تُبْتُ إِلَيْكَ وَأَنَا۠ أَوَّلُ ٱلْمُؤْمِنِينَ ﴿١٤٣﴾

*“Na alipofika Mussa katika miadi yetu na Mola wake akazungumza naye, (Mussa) akasema: “Mola wangu! Nioneshe (nafsi yako) ili nikuone” Akasema (Mwenyezi Mungu): “Hutaniona, lakini tazama jabali (lililoko mbele yako) kama litakaa mahali pake utaweza kuniona”. Basi Mola wake alipojionesha katika jabali, alilifanya liwe lenye kuvunjika vunjika na Mussa akaanguka hali ya kuzimia. Alipozindukana akasema “Utukufu ni wako. Natubu kwako, na mimi ni wa kwanza wa wanaoamini (haya)” (7:143).*

➢Pia tunafahamishwa katika Qur-an kuwa Bibi Maryam, mama wa Nabii Issa(a.s) naye aliongeleshwa nyuma ya pazia wakati wa kumzaa Masihi Issa Bin Maryamu kama ilivyo katika aya zifuatazo:

فَأَجَآءَهَا ٱلْمَخَاضُ إِلَىٰ جِذْعِ ٱلنَّخْلَةِ قَالَتْ يَٰلَيْتَنِى مِتُّ قَبْلَ هَٰذَا
وَكُنتُ نَسْيًا مَّنسِيًّا ﴿٢٣﴾

*“Kisha uchungu ukampeleka katika shina la mtende, (akawa anazaa na huku) anasema:“Laiti ningelikufa kabla ya haya, na ningekuwa niliyesahaulika kabisa.(19:23)*

فَنَادَىٰهَا مِن تَحۡتِهَآ أَلَّا تَحۡزَنِي قَدۡ جَعَلَ رَبُّكِ تَحۡتَكِ سَرِيّٗا ٢٤

*"Mara ikamfikia sauti kutoka chini yake ikamwambia usihuzunike. Hakika Mola wako amejaalia kijito cha maji chini yako'"(19:24)*

وَهُزِّيٓ إِلَيۡكِ بِجِذۡعِ ٱلنَّخۡلَةِ تُسَٰقِطۡ عَلَيۡكِ رُطَبٗا جَنِيّٗا ٢٥

*"Na litikise kwako shina la mtende, litakuangushia tende nzuri, zilizo mbivu". (19:25)*

فَكُلِي وَٱشْرَبِي وَقَرِّي عَيْنًا ۖ فَإِمَّا تَرَيِنَّ مِنَ ٱلْبَشَرِ أَحَدًا فَقُولِيٓ إِنِّي نَذَرْتُ لِلرَّحْمَٰنِ صَوْمًا فَلَنْ أُكَلِّمَ ٱلْيَوْمَ إِنسِيًّا ﴿٢٦﴾

*"Basi ule na unywe na litulie jicho (lako). Na kama ukimuona mtu yeyote (akauliza habari juu ya mtoto huyu), sema: "Hakika mimi nimeweka nadhiri kwa Mwingi wa Rehma ya kufunga, kwa hiyo leo sitasema na mtu" (19:26).*

## (c) Kutumwa Malaika na kufikisha ujumbe kama alivyotumwa

Kutuma ujumbe wa Malaika ni njia nyingine anayoitumia Allah(s.w) katika kuwaelimisha wanaadamu hasa katika mambo ya msingi ya maisha ya mwanaadamu hapa ulimwenguni. Hii ni njia maalum aliyoitumia Allah katika kuwasiliana na Mitume na miongoni mwa watu wengine wema. Kuhusu jinsi Mtume(s.a.w) alivyofundishwa na Allah(s.w) tunafahamishwa katika aya zifuatazo:

وَٱلنَّجْمِ إِذَا هَوَىٰ ۝١ مَا ضَلَّ صَاحِبُكُمْ وَمَا غَوَىٰ ۝٢ وَمَا
يَنطِقُ عَنِ ٱلْهَوَىٰٓ ۝٣

*Naapa kwa nyota zinapoanguka. (Zinapokuchwa). Kwamba mtu wenu (huyu Muhammad) hakupotea kwa ujinga wala hakukosa. (na hali ya kuwa anajua); wala hasemi kwa matamanio (ya nafsi yake). (53:1-3)*

إِنْ هُوَ إِلَّا وَحْيٌ يُوحَىٰ ﴿٤﴾ عَلَّمَهُۥ شَدِيدُ ٱلْقُوَىٰ ﴿٥﴾ ذُو مِرَّةٍ

فَٱسْتَوَىٰ ﴿٦﴾ وَهُوَ بِٱلْأُفُقِ ٱلْأَعْلَىٰ ﴿٧﴾

*"Hayakuwa haya (anayosema) ila ni wahyi (ufunuo). Uliofunuliwa (kwake) .Amemfundisha (malaika) mwenye nguvu sana mwenye uweza. Na yeye yu katika upeo wa kuona (Horizon) katika mbingu kwa juu kabisa".(53:4-6)*

ثُمَّ دَنَا فَتَدَلَّىٰ ﴿٨﴾ فَكَانَ قَابَ قَوْسَيْنِ أَوْ أَدْنَىٰ ﴿٩﴾ فَأَوْحَىٰٓ

إِلَىٰ عَبْدِهِۦ مَآ أَوْحَىٰ ﴿١٠﴾ مَا كَذَبَ ٱلْفُؤَادُ مَا رَأَىٰٓ ﴿١١﴾

أَفَتُمَـٰرُونَهُۥ عَلَىٰ مَا يَرَىٰ ﴿١٢﴾

*"Kisha (ukaribu wao) ni kama baina ya upinde na upinde au karibu zaidi. Na akamfunulia huyo Mtumwa wake (Mwenyezi Mungu) aliyoyafunua. Moyo haukusema uwongo uliyoyaona.(Moyo wake ulisadikisha haya yaliyotokea). Je! Mnabishana naye juu ya yale anayoyaona (daima)?" (53:7-12).*

- Katika mafunzo ya Qur-an na Hadithi tunafahamishwa kuwa malaika Jibril ndiye malaika mkuu aliyehusika na kupeleka ujumbe kwa Mitume wa Allah(s.w).
- Lakini pia kutokana na aya za Qur-an sio yeye pekee aliyehusika tu na kupeleka ujumbe wa Allah kwa Mitume bali malaika wengine pia walihusika.
- Katika aya zifuatazo tunafahamishwa juu ya wageni (wajumbe) wa Nabii Ibrahim(a.s):

waliomletea habari njema ya kumpata mtoto Is-haqa na habari ya kuhuzunisha ya kuangamizwa kwa watu waovu wa Kaumu ya Lut(a.s) aliyekuwa mpwawe:

وَنَبِّئْهُمْ عَن ضَيْفِ إِبْرَٰهِيمَ ﴿٥١﴾ إِذْ دَخَلُوا۟ عَلَيْهِ فَقَالُوا۟ سَلَٰمًا قَالَ إِنَّا
مِنكُمْ وَجِلُونَ ﴿٥٢﴾ قَالُوا۟ لَا تَوْجَلْ إِنَّا نُبَشِّرُكَ بِغُلَٰمٍ عَلِيمٍ ﴿٥٣﴾

*“Na uwaambie khabari za wageni wa (Nabii) Ibrahim. Walipoingia kwake na wakasema:“Salaam” (Salaamun Alaykum, akawajibu; kisha) akasema (alipoona wamekataa kula chakula alichowawekea). “Kwa hakika sisi tunakuogopeni”.Wakasema: “Usituogope, Sisi tunakupa khabari njema ya (kuwa utazaa) mtoto mwenye ilimu kubwa”. (15:51-53)*

قَالَ أَبَشَّرۡتُمُونِي عَلَىٰٓ أَن مَّسَّنِيَ ٱلۡكِبَرُ فَبِمَ تُبَشِّرُونَ ﴿٥٤﴾ قَالُواْ بَشَّرۡنَٰكَ
بِٱلۡحَقِّ فَلَا تَكُن مِّنَ ٱلۡقَٰنِطِينَ ﴿٥٥﴾ قَالَ وَمَن يَقۡنَطُ مِن رَّحۡمَةِ رَبِّهِۦٓ
إِلَّا ٱلضَّآلُّونَ ﴿٥٦﴾

*"Akasema: "Oh! Mnanipa khabari hii, na hali ya kuwa uzee umenishika! Basi kwa njia gani mnanipa khabari njema hiyo?" Wakasema: "Tumekupa khabari njema iliyo haki: basi usiwe miongoni mwa wanaokata tamaa". Akasema: "Na nani anayekata tamaa ya rehema ya Mola isipokuwa wale waliopotea?"(15:54-56)*

قَالَ فَمَا خَطْبُكُمْ أَيُّهَا ٱلْمُرْسَلُونَ ﴿٥٧﴾ قَالُوٓا۟ إِنَّآ أُرْسِلْنَآ إِلَىٰ

قَوْمٍ مُّجْرِمِينَ ﴿٥٨﴾

*Akasema: (Tena) kusudi lenu (jingine) ni nini enyi mliotumwa?” Wakasema: “Hakika sisi tumetumwa kwa wale watu wakosaji (tukawaangamize).(15:57-58)*

إِلَّآ ءَالَ لُوطٍ إِنَّا لَمُنَجُّوهُمْ أَجْمَعِينَ ﴿٥٩﴾ إِلَّا ٱمْرَأَتَهُۥ قَدَّرْنَآ ۙ إِنَّهَا
لَمِنَ ٱلْغَٰبِرِينَ ﴿٦٠﴾

*(Watu wa Nabii Lut.) "Isipokuwa waliomfuata Lut. Bila shaka sisi tutawaokoa wote hao (waliomfuata Lut)" Isipokuwa mkewe. Tunapimia ya kuwa atakuwa miongoni mwa watakaokaa nyuma (waangamizwe)".(15;59-60)*

فَلَمَّا جَآءَ ءَالَ لُوطٍ ٱلْمُرْسَلُونَ ﴿٦١﴾ قَالَ إِنَّكُمْ قَوْمٌ مُّنكَرُونَ ﴿٦٢﴾

*“Basi wajumbe walipofika kwa watu wa Lut (kwa sura za kibinaadamu). (Lut) alisema:“Hakika nyinyi ni watu msiojulikana (na mimi; sikujueni)”.(15:61-62).*

قَالُواْ بَلْ جِئْنَٰكَ بِمَا كَانُواْ فِيهِ يَمْتَرُونَ ﴿٦٣﴾ وَأَتَيْنَٰكَ بِٱلْحَقِّ وَإِنَّا

لَصَٰدِقُونَ ﴿٦٤﴾

*“Wakasema:“Basi sisi tumekuletea yale ambayo walikuwa wanayafanyia shaka, (nayo ni maangamizo yao)”.“Na tumefika kwako kwa (hilo jambo la) haki (la kuangamizwa) na hakika sisi ni wenye kusema kweli.(15:63-64)*

فَأَسْرِ بِأَهْلِكَ بِقِطْعٍ مِّنَ ٱلَّيْلِ وَٱتَّبِعْ أَدْبَـٰرَهُمْ وَلَا يَلْتَفِتْ مِنكُمْ أَحَدٌ

وَٱمْضُوا۟ حَيْثُ تُؤْمَرُونَ ﴿٦٥﴾ وَقَضَيْنَآ إِلَيْهِ ذَٰلِكَ ٱلْأَمْرَ أَنَّ دَابِرَ

هَـٰٓؤُلَآءِ مَقْطُوعٌ مُّصْبِحِينَ ﴿٦٦﴾

*"Basi ondoka na watu wako katika kipande cha usiku (pingapinga la usiku), na wewe ufuate nyuma yao; wala yeyote katika nyinyi asigeuke nyuma (na mwende upesi upesi) nakoamrishwa".Na tukamkatia (Nabii Luti) jambo hili; la kwamba mizizi yao itakatwa asubuhi (yaani wataangamiziliwa mbali asubuhi)"(15:65-66)*

Zakaria(a.s) mlezi wa Maryamu mama wa Nabii Issa(a.s) aliletewa habari na malaika ya kumzaa Yahya(a.s) kama tunavyofahamishwa katika aya zifuatazo:

هُنَالِكَ دَعَا زَكَرِيَّا رَبَّهُۥۖ قَالَ رَبِّ هَبۡ لِي مِن لَّدُنكَ ذُرِّيَّةً طَيِّبَةًۖ
إِنَّكَ سَمِيعُ ٱلدُّعَآءِ ٣٨ فَنَادَتۡهُ ٱلۡمَلَٰٓئِكَةُ وَهُوَ قَآئِمٞ يُصَلِّي فِي
ٱلۡمِحۡرَابِ أَنَّ ٱللَّهَ يُبَشِّرُكَ بِيَحۡيَىٰ مُصَدِّقَۢا بِكَلِمَةٖ مِّنَ ٱللَّهِ وَسَيِّدٗا
وَحَصُورٗا وَنَبِيّٗا مِّنَ ٱلصَّٰلِحِينَ ٣٩

*Pale pale Zakaria akamwomba Mola wake, akasema: "Mola wangu! Nipe kutoka kwako mtoto mwema. Wewe ndiye usikiaye maombi (ya wanaokuomba)". Mara Malaika wakamlingania hali amesimama akiswali chumbani, kwamba Mwenyezi Mungu anakupa khabari njema za (kuwa utazaa mtoto; umwite) Yahya, atakayekuwa mwenye kumsadikisha (Mtume atakayezaliwa) kwa neno litokalo kwa Mwenyezi Mungu (Naye ni Nabii Issa) na atakayekuwa bwana kabisa na mtawa na Nabii anayetokana na watu wema (Nao ni nyinyi).*

قَالَ رَبِّ أَنَّىٰ يَكُونُ لِي غُلَٰمٌ وَقَدْ بَلَغَنِيَ ٱلْكِبَرُ وَٱمْرَأَتِي عَاقِرٌ ۖ قَالَ

كَذَٰلِكَ ٱللَّهُ يَفْعَلُ مَا يَشَآءُ ﴿٤٠﴾

*"Akasema (Zakaria): "Mola wangu! Nitapataje mtoto, na hali uzee umenifikia, na mke wangu ni tasa?" Akasema (Mwenyezi Mungu), "Ndiyo vivyo hivyo; Mwenyezi Mungu hufanya apendavyo)".*

قَالَ رَبِّ ٱجۡعَل لِّيٓ ءَايَةٗۖ قَالَ ءَايَتُكَ أَلَّا تُكَلِّمَ ٱلنَّاسَ ثَلَٰثَةَ أَيَّامٍ إِلَّا
رَمۡزٗاۗ وَٱذۡكُر رَّبَّكَ كَثِيرٗا وَسَبِّحۡ بِٱلۡعَشِيِّ وَٱلۡإِبۡكَٰرِ ٤١

*“mke wangu kishashika mimba nipate kufurahi upesi)”. Akasema: “Alama yako ni kuwa hutaweza kusema na watu kwa siku tatu isipokuwa kwa ishara tu. Na mtaje Mola wako kwa wingi na umtukuze (kwa kuswali) wakati wa jioni na asubuhi”. (3:41)*

Pia Bibi Maryamu alileletewa ujumbe na malaika kutoka kwa Allah kama inavyodhihirika katika aya zifuatazo:

وَٱذۡكُرۡ فِي ٱلۡكِتَٰبِ مَرۡيَمَ إِذِ ٱنتَبَذَتۡ مِنۡ أَهۡلِهَا مَكَانٗا شَرۡقِيّٗا ﴿١٦﴾

فَٱتَّخَذَتۡ مِن دُونِهِمۡ حِجَابٗا فَأَرۡسَلۡنَآ إِلَيۡهَا رُوحَنَا فَتَمَثَّلَ لَهَا بَشَرٗا

سَوِيّٗا ﴿١٧﴾ قَالَتۡ إِنِّيٓ أَعُوذُ بِٱلرَّحۡمَٰنِ مِنكَ إِن كُنتَ تَقِيّٗا ﴿١٨﴾ قَالَ

إِنَّمَآ أَنَا۠ رَسُولُ رَبِّكِ لِأَهَبَ لَكِ غُلَٰمٗا زَكِيّٗا ﴿١٩﴾

*Na mtaje Mariamu Kitabuni (humu). Alipojitenga na jamaa zake, (akaenda) mahali upande wa mashariki (wa msikiti). Na akaweka pazia kujikinga nao. Tukampelekea Muhuisha Sharia yetu (Jibrili) - akajimithilisha kwake (kwa sura ya) binaadamu aliye kamili. (Mariamu) akasema: "Hakika mimi najikinga kwa (Mwenyezi Mungu) Mwingi wa rehema (Aniepushe) nawe. Ikiwa unamuogopa Mungu (basi ondoka nenda zako)." (Malaika) akasema: "Hakika mimi ni Mjumbe wa Mola wako: ili nikupe mwana mtakatifu" (19:16-19)*

- Pamoja na Malaika kuleta ujumbe kwa Mitume na miongoni mwa watu wema, pia kuna Malaika waliokuja kufundisha elimu ya uchawi kama sehemu ya mtihani kwa wanaadamu.
- Malaika waliotumwa na Allah kufundisha uchawi kama mtihani kwetu ni Haruta na Maruta kama inavyobainishwa katika Qur-an:

وَٱتَّبَعُوا۟ مَا تَتْلُوا۟ ٱلشَّيَـٰطِينُ عَلَىٰ مُلْكِ سُلَيْمَـٰنَ ۖ وَمَا كَفَرَ سُلَيْمَـٰنُ
وَلَـٰكِنَّ ٱلشَّيَـٰطِينَ كَفَرُوا۟ يُعَلِّمُونَ ٱلنَّاسَ ٱلسِّحْرَ وَمَآ أُنزِلَ عَلَى
ٱلْمَلَكَيْنِ بِبَابِلَ هَـٰرُوتَ وَمَـٰرُوتَ ۚ وَمَا يُعَلِّمَانِ مِنْ أَحَدٍ حَتَّىٰ يَقُولَآ
إِنَّمَا نَحْنُ فِتْنَةٌ فَلَا تَكْفُرْ ۖ فَيَتَعَلَّمُونَ مِنْهُمَا مَا يُفَرِّقُونَ بِهِۦ بَيْنَ ٱلْمَرْءِ
وَزَوْجِهِۦ ۚ وَمَا هُم بِضَآرِّينَ بِهِۦ مِنْ أَحَدٍ إِلَّا بِإِذْنِ ٱللَّهِ ۚ وَيَتَعَلَّمُونَ مَا
يَضُرُّهُمْ وَلَا يَنفَعُهُمْ ۚ وَلَقَدْ عَلِمُوا۟ لَمَنِ ٱشْتَرَىٰهُ مَا لَهُۥ فِى ٱلْـَٔاخِرَةِ مِنْ
خَلَـٰقٍ ۚ وَلَبِئْسَ مَا شَرَوْا۟ بِهِۦٓ أَنفُسَهُمْ ۚ لَوْ كَانُوا۟ يَعْلَمُونَ ﴿١٠٢﴾

*“Wakafuata yale waliyoyafuata mashetani, (wakadai kuwa yalikuwa) katika ufalme wa (Nabii) Suleiman, na Suleiman hakukufuru, bali mashetani ndio waliokufuru, wakiwafundisha watu uchawi na (uchawi) ulioteremshwa kwa Malaika wawili, Haruta na Maruta, katika (mji wa) Babil. Wala (Malaika hao) hawakumfundisha yeyote mpaka wamwambie: “Hakika sisi ni mtihani (wa kutazamwa kutii kwenu); basi usikufuru”. Wakajifunza kwao ambayo kwa mambo hayo waliweza kumfarikisha mtu na mkewe (na mengineyo).*

*Wala hawakuwa wenye kumdhuru yoyote kwa hayo ila kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na wanajifunza ambayo yatawadhuru wala hayatawafaa. Na kwa yakini wanajua kwamba aliyekhiari haya hatakuwa na sehemu yoyote katika akhera. Na bila shaka ni kibaya kabisa walichouzia (starehe za) nafsi zao (za akhera). Laiti wangalijua, (hakika wasingefanya hivi)". (2:102).*

- Aya hii inazidi kututhibitishia kuwa hapana chochote ambacho anakijua mwanaadamu ila itakuwa amefundishwa na Allah (s.w).

# (d) Ndoto za kweli(ndoto za Mitume)

- Njia nyingine ya kupata ujumbe kutoka kwa Allah ni njia ya ndoto za kweli.
- Historia inatuonyesha kuwa ndoto za Mitume daima zilikuwa zikitokea kweli; kwa hiyo ulikuwa ni ujumbe moja kwa moja kutoka kwa Allah(s.w).
- Ndio maana Nabii Ibrahim(a.s) alipoota kuwa anamchinja mwanawe, hakusita kutekeleza hilo kwa kuwa yeye na mtoto wake Ismail (a.s) walikuwa na uhakika kuwa ni amri kutoka kwa Allah kama inavyobaini katika Aya ifuatayo:

.............. قَالَ يَٰبُنَيَّ إِنِّيٓ أَرَىٰ فِي ٱلۡمَنَامِ أَنِّيٓ أَذۡبَحُكَ فَٱنظُرۡ مَاذَا تَرَىٰۚ

قَالَ يَٰٓأَبَتِ ٱفۡعَلۡ مَا تُؤۡمَرُۖ سَتَجِدُنِيٓ إِن شَآءَ ٱللَّهُ مِنَ ٱلصَّٰبِرِينَ ١٠٢

*"....................Ewe mwanangu! Hakika nimeona katika ndoto ya kwamba ninakuchinja. Basi fikiri, waonaje?" Akasema: "Ewe baba yangu! Fanya unayoamrishwa, utanikuta Insha-Allah miongoni mwa wanao subiri." (37:102)*

- Kutokea kweli kwa ndoto ya Nabii Yusuf(a.s) kama inavyobainishwa katika Qur-an ni miongoni mwa ushahidi kuwa ndoto za Mitume ni ujumbe wa kweli na wa moja kwa moja (kama ndoto yenyewe ilivyo) kutoka kwa Allah(s.w).
- Hebu turejee kisa cha ndoto ya Nabii Yusuf(a.s) katika aya zifuatazo:

إِذْ قَالَ يُوسُفُ لِأَبِيهِ يَٰٓأَبَتِ إِنِّى رَأَيْتُ أَحَدَ عَشَرَ كَوْكَبًا وَٱلشَّمْسَ

وَٱلْقَمَرَ رَأَيْتُهُمْ لِى سَٰجِدِينَ ﴿٤﴾

*“Kumbuka Yusuf alipomwambia baba yake: “Ewe baba yangu! Hakika nimeona katika ndoto nyota kumi na moja na jua na mwezi. Nimeviona vyote hivi vinanisujudia” (12:4)*

قَالَ يَٰبُنَيَّ لَا تَقۡصُصۡ رُءۡيَاكَ عَلَىٰٓ إِخۡوَتِكَ فَيَكِيدُواْ لَكَ كَيۡدًاۖ إِنَّ
ٱلشَّيۡطَٰنَ لِلۡإِنسَٰنِ عَدُوّٞ مُّبِينٞ ٥

*“Akasema (babaake): “Ewe mwanangu! Usiwasimulie ndoto yako (hii) nduguzo wasije wakakufanyia vitimbi (kwa ajili ya husda itakayowapanda). Hakika shetani kwa mwanaadamu ni adui aliye dhahiri (atawatia uchungu tu)”. (12:5)*

# Kutokea kweli kwa ndoto hii kunabainishwa katika aya ifuatayo:

وَرَفَعَ أَبَوَيْهِ عَلَى ٱلْعَرْشِ وَخَرُّوا۟ لَهُۥ سُجَّدًا ۖ وَقَالَ يَٰٓأَبَتِ هَٰذَا تَأْوِيلُ
رُءْيَٰىَ مِن قَبْلُ قَدْ جَعَلَهَا رَبِّى حَقًّا ۖ وَقَدْ أَحْسَنَ بِىٓ إِذْ أَخْرَجَنِى مِنَ
ٱلسِّجْنِ وَجَآءَ بِكُم مِّنَ ٱلْبَدْوِ مِنۢ بَعْدِ أَن نَّزَغَ ٱلشَّيْطَٰنُ بَيْنِى وَبَيْنَ
إِخْوَتِىٓ ۚ إِنَّ رَبِّى لَطِيفٌ لِّمَا يَشَآءُ ۚ إِنَّهُۥ هُوَ ٱلْعَلِيمُ ٱلْحَكِيمُ ﴿١٠٠﴾

*“(Na walipoingia kwa Yusuf), aliwainua wazazi wake na kuwaweka katika kiti (chake) cha ufalme. Na wote wakaporomoka kumsujudia.*
*Na (Yusuf) akasema: “Ewe babaangu! Hii ndiyo (tafsiri) hakika ya ndoto yangu ya zamani. Bila shaka Mola wangu ameihakikisha. Na amenifanyia ihsani akanitoa gerezani na akakuleteni nyinyi kutoka jangwani; baada ya shetani kuchochea baina yangu na ndugu zangu. Hakika Mola wangu ni mwenye kulifikia alitakalo. Bila shaka yeye ni mjuzi na mwenye hikima”. (12:100).*

- ➢Kutokea kweli kwa ndoto ya Mtume(s.a.w) kuwa Waislamu wataingia Makka kuhiji kwa salama bila ya kuzuiliwa na mtu yeyote.
- ➢Ndoto hii ilitokea kweli kama  unavyofahamishwa katika aya ifuatayo:

لَّقَدْ صَدَقَ ٱللَّهُ رَسُولَهُ ٱلرُّءْيَا بِٱلْحَقِّ ۖ لَتَدْخُلُنَّ ٱلْمَسْجِدَ ٱلْحَرَامَ إِن
شَآءَ ٱللَّهُ ءَامِنِينَ مُحَلِّقِينَ رُءُوسَكُمْ وَمُقَصِّرِينَ لَا تَخَافُونَ ۖ فَعَلِمَ مَا
لَمْ تَعْلَمُوا۟ فَجَعَلَ مِن دُونِ ذَٰلِكَ فَتْحًا قَرِيبًا ﴿٢٧﴾

*“Kwa yakini Mwenyezi Mungu amemhakikishia Mtume wake ndoto yake ya haki. Bila shaka nyinyi mtaingia katika Msikiti Mtukufu Insha-Allah kwa salama; mkinyoa vichwa vyenu na mkipunguza nywele (kama ilivyowajibu kufanya hivyo wakati wa Hija). Hamtakuwa na khofu. Na (Mwenyezi Mungu) anajua msiyoyajua. Basi kabla ya haya atakupeni kushinda kuliko karibu”. (48:27)*

**(e) Njia ya Maandishi(mbao zilizoandikwa tayari)**

- Njia nyingine anayoitumia Allah(s.w) katika kuwasiliana na waja wake ni njia ya maandishi, yaani maandishi yaliyoandikwa tayari.
- Nabii Mussa(a.s) aliletewa ujumbe kutoka kwa Allah(s.w) kwa maandishi yaliyoandikwa tayari katika mbao kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

وَكَتَبْنَا لَهُۥ فِى ٱلْأَلْوَاحِ مِن كُلِّ شَىْءٍ مَّوْعِظَةً وَتَفْصِيلًا لِّكُلِّ شَىْءٍ

فَخُذْهَا بِقُوَّةٍ.................

*"Na tukamwandikia katika mbao kila kitu mawaidha (ya kila namna) na maelezo ya kila jambo. Basi yashike kwa imara na uwaamrishe watu wako wayashike vema haya..." (7:145)*

وَلَمَّا سَكَتَ عَن مُّوسَى ٱلْغَضَبُ أَخَذَ ٱلْأَلْوَاحَ ۖ وَفِى نُسْخَتِهَا هُدًى وَرَحْمَةٌ لِّلَّذِينَ هُمْ لِرَبِّهِمْ يَرْهَبُونَ ﴿١٥٤﴾

*“Na Musa zilipotulia ghadhabu zake, aliziokota zile mbao. Na katika maandiko yake (hizo mbao) ulikuwamo uwongofu na rehema kwa wale wanaomuogopa Mola wao”. (7:154).*

- Kwa ujumla tumeona kuwa chanzo cha elimu ni “Allah(s.w). Lolote tunalolifahamu tumefunzwa na Allah kwa njia mojawapo katika njia tano tulizoziona.

**KATIKA UISLAMU HAKUNA ELIMU YA DINI NA DUNIA**

- Makafiri na hata baadhi ya Waislamu kutokana na mtazamo wao mfinyu juu ya maana ya dini iliyowapelekea kuyagawanya maisha ya binaadamu kwenye matapo mawili; maisha ya dini na maisha ya dunia, wameigawanya elimu kwenye matapo hayo mawili.

- Kwa mtazamo huu potofu elimu ya dini ni ile inayoshughulikia maswala ya kiroho (spiritual life) ya mtu binafsi inayoishia katika kumuwezesha mtu kuswali, kufunga na kutekeleza Ibada nyingine maalumu kama hizi bila ya kuzihusisha na maisha yake ya kila siku ya kibinafsi, kifamilia na kijamii.
- Hivyo elimu hii haina nafasi ya kumuwezesha binaadamu kuendea maisha yake ya kila siku ya kijamii.

- Elimu ya Dunia kwa mtazamo huu wa makafiri, ni ile inayojishughulisha na masuala ya kijamii kama vile uchumi, siasa, utamaduni, sheria na maongozi ya jamii kwa ujumla kwa kufuata maelekezo na matashi ya binaadamu bila ya kuzingatia mwongozo wa Allah(s.w).

- Kwa mtazamo wa mgawanyo huu, elimu ya dini ndiyo iliyofundishwa na Allah(s.w) kupitia kwa Mitume na Vitabu vyake na elimu ya dunia imebuniwa na binaadamu wenyewe kwa msukumo wa matashi na mahitaji yao katika kuendea kila kipengele cha maisha yao ya kimaada (Physical or Material life).

- Kwa mtazamo wa Uislamu (Qur-an na Sunnah) hapana mgawanyo huu wa elimu kwa sababu za msingi zifuatazo:

**Kwanza, Nabii Adam(a.s) katika kuandaliwa yeye na kikazi chake** kuwa Makhalifa wa Allah(s.w) hapa ulimwenguni alifundishwa majina ya vitu vyote kama Qur-an inavyoainisha:

وَعَلَّمَ ءَادَمَ ٱلْأَسْمَآءَ كُلَّهَا

*“Na (Mwenyezi Mungu) akamfundisha Adam majina ya vitu vyote…” (2:31).*

- Majina ya vitu vyote hapa inaashiria fani zote za elimu zitakazomuwezesha binaadamu kuendea kila kipengele cha maisha yake na kufikia malengo tarajiwa.
- Pamoja na kufundishwa majina ya vitu vyote, pia Adam(a.s) na kizazi chake waliahidiwa na Mola wao kuletewa mwongozo utakaowawezesha kutumia fani mbali mbali za taaluma walizonazo kwa kufuata utaratibu utakaowapelekea kukiendea kila kipengele cha maisha yao kwa furaha na amani:

قُلْنَا ٱهْبِطُوا۟ مِنْهَا جَمِيعًا ۖ فَإِمَّا يَأْتِيَنَّكُم مِّنِّى هُدًى فَمَن تَبِعَ هُدَاىَ فَلَا

خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿٣٨﴾

*“Tukasema: Shukeni humo nyote; na kama ukikufikieni uwongozi utokao kwangu, basi watakaofuata uwongozi wangu huo, haitakuwa khofu juu yao wala hawatahuzunika.” (2:38).*

- Lakini wale watakaotumia taaluma mbali mbali walizonazo katika kuendea kila kipengele cha maisha yao ya kila siku ya kibinafsi na kijamii bila ya kufuata mwongozo wa Allah(s.w) kupitia kwa Mitume wake na Vitabu vyake, wataishi maisha ya huzuni na khofu na katika maisha ya akhera watakuwa na adhabu kali:

وَٱلَّذِينَ كَفَرُوا۟ وَكَذَّبُوا۟ بِـَٔايَـٰتِنَآ أُو۟لَـٰٓئِكَ أَصْحَـٰبُ ٱلنَّارِ ۖ هُمْ فِيهَا خَـٰلِدُونَ ٣٩

*“Lakini wenye kukufuru na kuyakadhibisha maneno yetu, hao ndio watakaokuwa watu wa motoni, humo watakaa milele.” (2:39)*

- Kwa mujibu wa maelezo haya tunajifunza kuwa fani zote za elimu (majina ya vitu vyote) ambazo amezifundisha Allah(s.w) pamoja na mwongozo maalumu kutoka kwake, vinahitajika kwa binaadamu ili kumuwezesha kuishi maisha ya furaha na amani hapa duniani na huko akhera.
- Hivyo hapana mwenye uwezo wa kutenganisha maisha ya dini na dunia au elimu ya dini na dunia.

**Pili, Amri ya kusoma (kutafuta elimu) aliyopewa Mtume (s.a.w) na** umma wake, haibagui elimu ya dini na dunia. Vinginevyo fani yoyote ya elimu inayomuwezesha binaadamu kusimamisha ukhalifa wa Allah(s.w) katika jamii na kufikia lengo la kuumbwa la kumuabudu Allah(s.w) inavyostahiki katika kila kipengele cha maisha yake inapaswa isomwe kwa juhudi zote.

**Tatu, chanzo cha fani zote za elimu ni Allah(s.w) kama Qur-an** inavyosisitiza:

ٱقۡرَأۡ وَرَبُّكَ ٱلۡأَكۡرَمُ ﴿٣﴾ ٱلَّذِى عَلَّمَ بِٱلۡقَلَمِ ﴿٤﴾ عَلَّمَ ٱلۡإِنسَـٰنَ مَا لَمۡ يَعۡلَمۡ ﴿٥﴾

*"Soma na Mola wako ni karimu sana. Ambaye amemfundisha (Binaadamu fani zote za elimu) kwa msaada wa kalamu. Amemfundisha mwanaadamu (chungu ya mambo) aliyokuwa haya jui". (96:3-5)*

- Kwa mujibu wa aya hizi hapana fani yoyote ya taaluma iliyoasisiwa na binaadamu.
- Hivyo suala la kuwa na elimu ya dunia iliyoasisiwa na binaadamu na elimu ya dini ambayo tu ndiyo iliyotoka kwa Allah (s.w), halipo kwa mtazamo wa Qur-an.

**Nne, katika Qur-an tunafahamishwa kuwa wanaomcha Allah(s.w)** ipasavyo na kumuogopa ni wale wataalamu (ulamaa) waliozama katika fani mbali mbali za elimu. Kwa mujibu wa Qur-an fani hizi mbali mbali haziishii tu kwenye zile fani zinazotazamwa kwa mrengo wa kidini kama vile fiqh Tawhiid, n.k. bali fani zote za elimu zinazo muwezesha binaadamu kutafakari kwa undani juu ya kuwepo Allah(s.w) na utukufu wake, hasa zile fani za kisayansi zinazohusiana na maumbile. Hebu turejee aya zifuatazo:

أَلَمْ تَرَ أَنَّ ٱللَّهَ أَنزَلَ مِنَ ٱلسَّمَآءِ مَآءً فَأَخْرَجْنَا بِهِۦ ثَمَرَٰتٍ مُّخْتَلِفًا أَلْوَٰنُهَا ۚ
وَمِنَ ٱلْجِبَالِ جُدَدٌۢ بِيضٌ وَحُمْرٌ مُّخْتَلِفٌ أَلْوَٰنُهَا وَغَرَابِيبُ سُودٌ ﴿٢٧﴾

*"Je! Huoni kwamba Mwenyezi Mungu ameteremsha maji toka mawinguni! Na kwayo tumeyatoa matunda yenye rangi mbali mbali. Na katika milima imo mistari myeupe na myekundu yenye rangi mbali mbali, na (mengine) myeusi sana". (35:27)*

وَمِنَ ٱلنَّاسِ وَٱلدَّوَآبِّ وَٱلْأَنْعَـٰمِ مُخْتَلِفٌ أَلْوَٰنُهُۥ كَذَٰلِكَ ۗ إِنَّمَا

يَخْشَى ٱللَّهَ مِنْ عِبَادِهِ ٱلْعُلَمَـٰٓؤُا۟ ۗ إِنَّ ٱللَّهَ عَزِيزٌ غَفُورٌ ٢٨

*Na katika watu na wanyama wanaotambaa na wanyama (wengine), pia rangi zao ni mbali mbali. Kwa hakika wanaomwogopa Mwenyezi Mungu miongoni mwa waja Wake ni wale wataalamu (wanavyuoni). Bila shaka Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Msamehevu. (35:28)*

- Katika aya hizi tunajifunza kuwa wenye kumcha Allah(s.w) ipasavyo na katika kiwango cha juu cha unyenyekevu ni wale waumini waliobobea katika taaluma mbali mbali (maulamaa).
- Je, maulamaa waliotajwa katika aya hizi ni wale tu waliobobea kwenye taaluma zinazoitwa za kidini kama vile fiq-h, Qur-an na Hadith? Maulamaa waliopigiwa mfano katika aya hizi ni wale waliozama katika fani ya Hali ya Hewa (Meteorologist),

Maulama waliozama katika uchunguzi wa wanyama (Zoologist), maulamaa waliozama katika fani ya matunda (Horticulturist), Maulamaa waliozama katika fani ya miamba (Geologists) na Maulamaa waliozama katika fani ya kuchunguza watu walivyo kimaumbile, rangi, n.k. (Anthropologist).

- Pia katika aya nyingi za Qur-an binaadamu amesisitizwa kuyafanyia utafiti mazingira ya mbingu na ardhi ili kumtambua Mola wake na kumuabudu ipasavyo.

**Tano, katika Qur-an Allah(s.w) anatufahamisha kuwa waumini** waliobobea kwenye elimu wana daraja kubwa zaidi kuliko waumini wengine:

يَرْفَعِ ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ مِنكُمْ وَٱلَّذِينَ أُوتُوا۟ ٱلْعِلْمَ ................
دَرَجَٰتٍ ۚ وَٱللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ ﴿١١﴾

*"..........................Mwenyezi Mungu atawainua wale walioamini miongoni mwenu; na waliopewa elimu watapata daraja zaidi. Na Mwenyezi Mungu anazo habari za mnayoyatenda yote." (58:11)*

- Aya hii haijabagua wenye elimu.
- Hivyo yeyote yule mwenye taaluma inayomuwezesha kumcha Mola wake na kumuabudu inavyostahiki katika kila kipengele cha maisha yake na ikamuwezesha kuchangia katika kusimamisha Uislamu katika jamii atakuwa na daraja zaidi kuliko wale wasio na taaluma hiyo kama Qur-an inavyozidi kusisitiza:

إِنَّ أَكْرَمَكُمْ عِندَ ٱللَّهِ أَتْقَىٰكُمْ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ عَلِيمٌ خَبِيرٌ ﴿١٣﴾

*“……………… Hakika ahishimiwaye sana miongoni mwenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni yule amchaye Mwenyezi Mungu zaidi katika nyingi.” (49:13)*

**Sita, hatuoni mgawanyo wa elimu katika Hadith mbali mbali za** Mtume(s.a.w) zinazozungumzia elimu. Kwa mfano Mtume (s.a.w) aliposema: “Kutafuta elimu ni faradhi kwa kila Muislamu mwanamume na kila Muislamu mwanamke.” (Ibn Majah), hakubagua elimu. Pia rejea Hadith zifuatazo:

*Anas (r.a) ameeleza kuwa Mtume (s.a.w) amesema: Mwenye kutoka nje kutafuta elimu yuko katika njia ya Allah mpaka atakapo rejea. (Tirmidh).*

*Abu Hurairah (r.a) aemeeleza kuwa Mtume (s.a.w) amesema:Yeyote atakayeulizwa juu ya jambo alilojifunza kisha akaficha (akakataa kutoa elimu ile) atavalishwa mshipi (mkanda) wa Moto siku ya Kiyama." (Ahmad, Abu Daud, Tirmidh na Ibn Majah).*

- Pia tunajifunza katika historia kuwa Mtume(s.a.w) aliwaacha huru mateka wa vita vya Badr kwa yule aliyeweza kujikomboa kwa kuwafunza kusoma na kuandika watoto kumi wa Waislamu.

- Hadithi hizi zinadhihirisha kuwa Mtume(s.a.w) naye hakuigawanya elimu katika elimu ya dini na elimu ya dunia.
- Uislamu umewahimiza Waislamu kutafuta elimu yenye manufaa kwa jamii popote pale inapopopatikana.

Hivyo, kutokana na hoja hizi sita, Uislamu hautambui mgawanyo wa
elimu kwenye tapo la ***elimu ya dini na elimu ya dunia.***

# Mgawanyo wa Elimu katika Faradh ‘Ain na Faradh Kifaya

Faradh ya elimu inaweza kugawanywa kwenye faradhi ‘Ain na faradh Kifaya. Faradh ‘Ain ni faradh inayomhusu kila mtu binafsi isiyo na uwakilishi. Mfano, kusimamisha swala, kutoa Zakat, kufunga, n.k. Ni katika faradh ‘ain.

- Faradh Kifaya ni faradh inayoweza kufanywa kwa uwakilishi.
- Ni faradhi ya kijamii.
- Wachache wanaweza kuitekeleza kwa niaba ya jamii.
- Kwa mfano swala ya maiti na yale yote ya faradh anayostahiki kufanyiwa maiti ya Kiislamu ni katika faradh kifaya.

- Elimu ya Maarifa ya Uislamu, itakayompelekea mja kumtambua, Mola wake, vilivyo na kumuabudu inavyostahiki katika kila kipengele cha maisha ni faradh ‘Ain.
- Kwa maana nyingine ni faradh kwa kila Muislamu kuujua Uislamu vilivyo na kujitahidi kuutekeleza kwa kadiri ya uwezo wake katika kila kipengele cha maisha.

- Elimu juu ya fani mbalimbali zinazohitajika katika maisha ya jamii ni faradhi kifaya kwa jamii ya Kiislamu. Kwa mfano ni faradhi kwa jamii ya Kiislamu kuwa na madaktari, wahandisi, wanasheria, wanasiasa, wanauchumi, waalimu na wataalamu wengineo katika kila fani ya maisha ya jamii wa kutosha kukidhi mahitajio ya jamii katika kuendea nyanja zote za maisha.

- Ikitokezea Waislamu wamezembea kiasi cha kushindwa kutoa wataalamu wanaohitajika kuendesha kila fani ya maisha ya jamii mpaka inapelekea Waislamu kushindwa kumuabudu Mola wao ipasavyo katika kipengele cha maisha, jamii yote ya Waislamu itakuwa katika lawama (itapata dhambi) na itaathirika kutokana na dhambi hii.

- Hivyo ili Waislamu waweze kusimamisha Uislamu (Ukhalifa wa Allah) katika jamii, kila Muislamu hanabudi kuufahamu Uislamu vilivyo na pawekwe mazingira ya makusudi yatakayomuwezesha kila Muislamu kujielimisha katika fani maalumu ya maisha inayohitajika katika jamii kwa kadiri ya vipaji alivyoruzukiwa na Mola wake.

- Kwa maana nyingine kila Muislamu mwenye vipaji vya kuwa Daktari au Mhandisi au Mwanasheria au Mchumi au Mwalimu au …. ajizatiti kuiendea taaluma hiyo na jamii ijizatiti kumuwezesha.
- Endapo, kwa mfano Muislamu mwenye kipaji cha kuwa Daktari, akazembea asiwe Daktari atakuwa mas-uli mbele ya Allah (s.w).
- Pia endapo jamii ya Waislamu itazembea isitoe Madaktari wanaohitajika itakuwa mas-uli mbele ya Allah (s.w).

# Elimu yenye Manufaa

- Elimu yenye manufaa ni ile ambayo:

**Kwanza, humuwezesha mja kufikia lengo la elimu. Tumeona kuwa** elimu imekuwa faradhi ya kwanza kwa waumini kwa kuwa elimu ndio nyenzo kuu ya kuwawezesha binaadamu kufikia lengo la kuumbwa kwao ambalo ni kumuabudu Allah (s.w), ipasavyo katika kila kipengele cha maisha yao. (Qur-an 51:56). Pia elimu ndio nyenzo kuu ya kuwawezesha waumini kuwa viongozi wa jamii (makhalifa wa Allah) katika ardhi. (Qur-an 2:30 - 31).

Elimu itakayotafutwa kinyume na kumuwezesha mtu kumuabudu Mola wake ipasavyo na kusimamamisha ukhalifa wa Allah(s.w) katika ardhi itakuwa si elimu yenye manufaa bali elimu yenye kuhasirisha kama tunavyojifunza katika hadithi zifuatazo:

*Abu Hurairah amesimulia kuwa Mtume (s.a.w) amesema: "Anayetafuta elimu isiyokuwa kwa ajili ya kutafuta radhi za Allah (s.w), hasomi kwa lengo lolote lile ila la kupata maslahi ya hapa duniani tu. Hivyo siku ya kiyama hatapata hata harufu ya Pepo." (Ahmad, Abu Daud, Ibn majah).*

*Pia Mtume(s.a.w) ametuasa kuwa mwenye kutafuta elimu ili awazidi wasome wengine au ili kuitumia katika biashara za kijahili au ili kujionesha kwa watu kuwa naye ni msomi, Mwenyezi Mungu atamuingiza motoni. (Tirmidh).*

**Pili, elimu yenye manufaa kwa binaadamu hapa ulimwenguni na** huko akhera ni ile ambayo pamoja na mtu binafsi kuitumia katika kumuabudu Allah(s.w) ipasavyo katika maisha yake ya kila siku, huifundisha au huifikisha kwa wengine pia kwa ajili ya kutafuta radhi za Allah(s.w).

- Ni vibaya mno mbele ya Allah(s.w) mtu kukataa au kuacha kufikisha kwa wengine kila anachokijua kama tunavyojifunza katika hadithi ifuatayo:

*“Abu Hurairah amesimulia kuwa Mtume (s.a.w) amesema: “Atakayeulizwa juu ya jambo alilojifunza kisha akaficha (akakataa kutoa elimu ile) atavalishwa mshipi wa moto katika siku ya Kiyama”. (Ahmad, Ibn Majah, Tirmidh na Abu Daud).*

- Katika hadith nyingine iliyosimuliwa na Abu Hurairah Mtume wa Allah (s.a.w) amesema:

*“Mfano wa elimu isiyonufaisha ni sawa na mfano wa mali iliyokusanywa bila ya kutumiwa katika njia ya Allah”. (Ahmad, Darini).*

- Kutokana na hadith hizi tunajifunza kuwa elimu yenye kunufaisha ni ile iliyofundishwa na wengine kinadharia na matendo.
- Kwa kufundisha watu unachokijua bila ya wewe mwenyewe kutenda ni mfano mbaya mno kwa wale wanaofundisha na chukizo kubwa mno mbele ya Allah (s.a.w):

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ لِمَ تَقُولُونَ مَا لَا تَفۡعَلُونَ ﴿٢﴾ كَبُرَ مَقۡتًا عِندَ
ٱللَّهِ أَن تَقُولُواْ مَا لَا تَفۡعَلُونَ ﴿٣﴾

*“Enyi mlioamini mbona mnasema msiyoyatenda? Ni chukizo kubwa mbele ya Allah(s.w) kusema msiyoyatenda.” (61:2-3)*

# Zoezi la 1:1

1. Nini maana ya Tawhiid kilugha na kisheria”
2. Ainisha aina tatu za Tawhiid.
3. Kinyume cha Tawhiid ni ________________________
4. (a) Elimu ni nini na nani aliyeelimika?

(b) (*“Sema, Je wanaweza kuwa sawa wale wanaojua na wale wasiojua)?........... (39:9).*

Ni kwa sababu gani wanaojua hawawi sawa na wasiojua?

(c) Unatoa maoni gani iwapo wanaojua na wasiojua watakuwa sawa
katika utendaji?

5. Toa maelezo yenye ushahidi wa Qur’an kuonesha kuwa:
(a) Elimu ndiyo takrima ya kwanza aliyotunukiwa binadamu na Mola wake.
(b) Kutafuta elimu kwa ajili ya Allah(s.w) ni faradh ya kwanza kwa Waislamu.
6. (a) Onesha kwa ushahidi wa Qur’an kuwa katika Uislamu mgawanyo wa elimu katika “elimu ya dunia” na “elimu ya Dini” haukubaliki.
(b) Kwa kurejea Qur’an onesha kuwa katika Uislamu kuna:
(i) Elimu ya Mwongozo.
(ii) Elimu ya Mazingira.

7. *“Soma kwa jina la Mola wako aliyeumba. Amemuumba mwanaadamu kwa ‘Alaq. Soma na Mola wako ni karimu sana. Ambaye amefundisha kwa msaada wa kalamu. Amemfundisha mwanaadamu mambo aliyokuwa hayajui”. (96:1-5).* (a) Nini maana ya “kusoma kwa jina la Allah(s.w)”?

(b) Orodhesha njia tano anazozitumia Allah(s.w) katika kuwaelimisha binadamu.

8. Elimu yenye manufaa kwa binadamu ni ile _____.

9. Kwanini elimu katika Uislamu imepewa nafasi ya kwanza. Toa sababu mbili (2).

# MTAZAMO WA UISLAMU JUU YA DINI

**Maana ya Dini**

“***Dini” ni suala la msingi sana kwa wanaadamu. Hata wale wanaodai*** kuwa hawana “Dini”, hawana namna ya kutohusiana na “***Dini”. Neno Dini*** limefasiriwa kwa mitazamo miwili tofauti:

(a) Mtazamo wa Makafiri juu ya Maana ya Dini

(b) Mtazamo wa Uislamu juu ya Maana ya Dini

## (a) Mtazamo wa Makafiri Juu ya Maana ya Dini.

- Kafiri Mutlaq (Kafiri hasa) ni yule anayekanusha moja kwa moja kuwepo kwa Allah(s.w), kuwepo siku ya mwisho na nguzo zote za Imani zilizosalia.
- Kwa mujibu wa Qur’an, Kafiri ni yule anayekanusha kiutendaji maamrisho ya Allah(s.w) yaliyobainishwa wazi katika vitabu vyake na Mitume wake. Anasema Allah(s.w) katika Qur’an:

وَمَن لَّمْ يَحْكُم بِمَآ أَنزَلَ ٱللَّهُ فَأُو۟لَـٰٓئِكَ هُمُ ٱلْكَـٰفِرُونَ ﴿٤٤﴾

*"Na wasiohukumu kwa yale aliyoteremsha Allah, basi hao ndio Makafiri" (5:44).*

- Makafiri wanainasibisha Dini na imani ya kuwepo Mungu Muumba. Katika kamusi ya Kiingereza chini ya neno "*Religion*" *– neno Dini* limefasiriwa hivi:

*“Belief in the existence of a supernatural ruling power, the creator and controller of the universe, who has given to Man a spiritual nature which continues to exist after the death of the body”1*

**Tafsiri:**

*Dini ni Imani ya kuwepo Mungu Muumba aliyemuweza na mwenye nguvu juu ya kila kitu. Mmiliki wa Ulimwengu, ambaye amempa binaadamu roho ambayo huendelea kuishi baada ya kifo cha mwili”.*

- Na katika kamusi ya Kiswahili sanifu, neno “Dini’ limefasiriwa ifuatavyo:

*“Imani inayohusiana na mambo ya kiroho baina ya binaadamu na Mwenyezi Mungu, au njia ya kuhusiana na Mwenyezi Mungu”*

- Katika kamusi hizi, Dini imenasibishwa na Imani ya kuwepo Allah(s.w). Kutokana na tafsiri hii ya neno “Dini”, makafiri ambao hawaamini kuwepo kwa Allah(s.w), wamedai kuwa wao hawana Dini.
- Lenin, miongoni mwa wanachuoni wa kikafiri anasisitiza katika kitabu chake “Socialism and Religion” (Ujamaa na Dini) kuwa:

*“Everybody must be absolutely free to profess any religion he pleases or no religion whatever, i.e. to be an atheist which every, socialist is as a rule…”*

*“Kila mtu hana budi kuwa huru kabisa kufuata Dini yoyote anayotaka au asiwe na Dini kabisa, yaani awe kafiri jambo ambalo inambidi kila mjamaa awe hivyo.”*

- Kutokana na maneno haya ya Lenin, mjamaa halisi au mkomunisti ni yule asiye na "Dini" kwa maana kwamba haamini kuwepo kwa Allah(s.w).
- Hivyo huendesha maisha yake ya kila siku kwa kufuata miongozo na matashi ya Watu.
- Kwa maana hii nchi zote za Kisekula; zinazodai kuwa hazina "*Dini*" ni za Kikafiri.

## (b) Mtazamo wa Uislamu Juu ya Maana ya Dini.

"Dini" ni neno la Kiarabu lenye maana zifuatazo:

(1) Uwezo au Mamlaka au Utawala.

(2) Itikadi na njia ya maisha.

(3) Kila Mila au mfumo wa maisha unaofuatwa na jamii ya Watu.

(4) Siku ya malipo (mfumo wa maisha ya akhera).

➢Katika Qur’an, neno Dini limetumika kwa maana zote hizi. Hebu turejee aya chache kama mfano:

➢Katika sura ya 3 aya ya 83 Allah(s.w) anauliza:

أَفَغَيْرَ دِينِ ٱللَّهِ يَبْغُونَ وَلَهُۥٓ أَسْلَمَ مَن فِى ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ طَوْعًا
وَكَرْهًا وَإِلَيْهِ يُرْجَعُونَ ﴿٨٣﴾

*“Je, (watu) wanataka Dini isiyokuwa ya Allah na hali kila kilichomo mbinguni na ardhini kimejisalimisha kwake kipende kisipende. Na kwake watarejeshwa wote” (3:83).*

- **Aya hii inatupa mafundisho makubwa matatu:**

**Kwanza: Swali “Je, wanataka Dini isiyokuwa ya Allah?” Linatupa** fundisho kuwa kuna Dini nyingi lakini anayostahiki aichague mwanaadamu ni ile ya Allah(s.w) ambayo hufuatwa na kila kilichomo mbinguni na ardhini bila ya hiari. Kwa maana nyingine mwanaadamu japo ana hiari ya kufuata au kutofuata Dini ya Allah (s.w), hana hiari ya kuishi bila ya Dini yoyote.

**Pili: Kwa ujuzi wa Sayansi uliopo, Dini ya kila kilichomo mbinguni na** ardhini si nyingine bali ni ile ya kujisalimisha kwa unyenyekevu kwa Allah (s.w). Kwa maana nyingine kila kilichomo mbinguni na ardhini ikiwa ni pamoja na mimea, wanyama, dunia yenyewe na sayari nyingine, jua, nyota na kila kilichomo katika anga, hufuata bila ya hiari sheria madhubuti alizoziweka Muumba Karima yaani Sheria za maumbile (natural laws).

- Hivyo katika aya hii neno Dini limetumika kwa maana ya utaratibu au mfumo wa maisha. Hivyo aya ya 3:83 tunaweza kuifasiri hivi:

*“Je, watu wanataka mfumo mwingine wa maisha usiokuwa ule alioweka Allah(s.w) na ili hali kila kilichomo mbinguni na ardhini kinafuata mfumo huo bila ya hiari……….”*

**Tatu: Sehemu ya mwisho ya aya hii, "*Na kwake watarejeshwa wote*",** inasisitiza kuwa japo wanaadamu wana hiari ya kuchagua utaratibu mwingine wa maisha usio kuwa ule alioupanga Allah(s.w), si stahiki yao na wala si hiari kiasi hicho bali ni mtihani kwao. Wote, baada ya maisha haya,watarejeshwa kwa Allah(s.w) na wote watahukumiwa kulingana na uamuzi wao kuhusu Dini.

- Waliofuata Dini ya Allah(s.w) pamoja na kupata mafanikio mazuri hapa duniani, watapata mafanikio mazuri zaidi huko Akhera; na wale waliounda Dini zao na kuzifuata, pamoja na migogoro ya maisha watakayoipata hapa duniani, huko akhera watastahiki kupata adhabu kali mno. Hili linasisitizwa katika aya ifuatayo:

وَمَن يَبْتَغِ غَيْرَ ٱلْإِسْلَٰمِ دِينًا فَلَن يُقْبَلَ مِنْهُ وَهُوَ فِى ٱلْءَاخِرَةِ مِنَ ٱلْخَٰسِرِينَ ﴿٨٥﴾

*"Na anayetaka Dini isiyokuwa Uislamu basi hatakubaliwa kwake. Naye Akhera atakuwa katika wenye khasara (kubwa kabisa)" (3:85).*

Katika sura ya 9 aya ya 33 na sura ya 61 aya ya 9 tunafahamishwa hivi:

هُوَ ٱلَّذِىٓ أَرْسَلَ رَسُولَهُۥ بِٱلْهُدَىٰ وَدِينِ ٱلْحَقِّ لِيُظْهِرَهُۥ عَلَى ٱلدِّينِ

كُلِّهِۦ وَلَوْ كَرِهَ ٱلْمُشْرِكُونَ ﴿٣٣﴾

*"Yeye ndiye aliyemleta Mtume wake kwa uongofu na Dini ya haki ili ajaalie kushinda Dini zote ijapokuwa watachukia washirikina" (9:33) (61:9).*

- Neno Dini hapa limetumika kwa maana ya utaratibu wa maisha. Vile vile katika aya hii tunajifunza mengi juu ya Dini:

**Kwanza, tunajifunza kuwa Dini ziko nyingi lakini iliyo ya haki ni moja** tu na hii ni ile iliyofundishwa na kufuatwa katika maisha ya kila siku na Mitume wa Allah(s.w).

**Pili, Dini au utaratibu wa maisha uliofumwa na Allah(s.w) na kufuatwa** na Mitume na wale walioamini pamoja nao, daima utakuwa juu ya mifumo mingine yote ya maisha iwapo itasimamishwa vilivyo.

**Tatu, tunajifunza kuwa, kuchukia kwa Washirikina Dini ya haki**
itakapokuwa juu, ina maana kuwa ushirikina nao ni Dini au mfumo wa maisha unaowaongoza washirikina katika kila kipengele cha maisha yao. Ingelikuwa Dini hii ya haki inajihusisha tu na vitendo fulani fulani vya dharura ambavyo waumini wake humfanyia Allah(s.w) tu bila kuhusisha maisha ya wanaadamu bila shaka washirikina wasingalichukia.

Lakini ilivyo ni kwamba, Dini ya Allah ni mfumo wa maisha unaosimamisha haki katika jamii na kutokomeza batili au dhulma; ambapo mfumo wa ushirikina umefumwa na watu kwa lengo la kuwadhulumu watu kwa kutumia majina ya miungu bandia. Kwa hiyo Dini ya haki ikisimama ushirikina hauna nafasi tena.

- Allah(s.w) katika aya kadhaa za Qur'an amelitumia neno Dini kwa maana ya mila na akatumia mila kwa maana ya Dini. Rejea kwa

إِنَّهُمْ إِن يَظْهَرُوا۟ عَلَيْكُمْ يَرْجُمُوكُمْ أَوْ يُعِيدُوكُمْ فِى مِلَّتِهِمْ وَلَن تُفْلِحُوٓا۟

إِذًا أَبَدًا ﴿٢٠﴾

*"Kwani wao wakikujueni mlipo watakupigeni mawe au watakurudisheni katika* ***mila yao; na hapo hamtafaulu abadan" (18:20).***

وَجَٰهِدُواْ فِي ٱللَّهِ حَقَّ جِهَادِهِۦۚ هُوَ ٱجۡتَبَىٰكُمۡ وَمَا جَعَلَ عَلَيۡكُمۡ فِي ٱلدِّينِ
مِنۡ حَرَجٖۚ مِّلَّةَ أَبِيكُمۡ إِبۡرَٰهِيمَۚ هُوَ سَمَّىٰكُمُ ٱلۡمُسۡلِمِينَ مِن قَبۡلُ وَفِي هَٰذَا
لِيَكُونَ ٱلرَّسُولُ شَهِيدًا عَلَيۡكُمۡ وَتَكُونُواْ شُهَدَآءَ عَلَى ٱلنَّاسِۚ فَأَقِيمُواْ
ٱلصَّلَوٰةَ وَءَاتُواْ ٱلزَّكَوٰةَ وَٱعۡتَصِمُواْ بِٱللَّهِ هُوَ مَوۡلَىٰكُمۡۖ فَنِعۡمَ ٱلۡمَوۡلَىٰ وَنِعۡمَ
ٱلنَّصِيرُ ٧٨

*“Na ipiganieni Dini ya Mwenyezi Mungu kama inavyostahiki (kupiganiwa). Yeye amekuchagueni (muwe uma ulio bora). Wala hakuweka juu yenu mambo mazito katika Dini. (Nayo Dini hii) ni* ***mila*** *ya baba yenu Ibrahim; yeye (Mwenyezi Mungu) alikwiteni Waislamu tangu (katika Vitabu vya zamani) huko na katika (Qur’an) hii pia (mmeitwa jina hilo) ili awe Mtume shahidi juu yenu na nyinyi muwe mashahidi juu ya watu (waliotangulia)’ (22:78).*

إِنَّ إِبْرَٰهِيمَ كَانَ أُمَّةً قَانِتًا لِّلَّهِ حَنِيفًا وَلَمْ يَكُ مِنَ ٱلْمُشْرِكِينَ ﴿١٢٠﴾
شَاكِرًا لِّأَنْعُمِهِ ۚ ٱجْتَبَىٰهُ وَهَدَىٰهُ إِلَىٰ صِرَٰطٍ مُّسْتَقِيمٍ ﴿١٢١﴾ وَءَاتَيْنَٰهُ فِى
ٱلدُّنْيَا حَسَنَةً ۖ وَإِنَّهُۥ فِى ٱلْءَاخِرَةِ لَمِنَ ٱلصَّٰلِحِينَ ﴿١٢٢﴾ ثُمَّ أَوْحَيْنَآ إِلَيْكَ
أَنِ ٱتَّبِعْ مِلَّةَ إِبْرَٰهِيمَ حَنِيفًا ۖ وَمَا كَانَ مِنَ ٱلْمُشْرِكِينَ ﴿١٢٣﴾

*“Hakika Ibrahiim alikuwa Imamu (mfano mzuri wa wema wa kuigwa) mnyenyekevu kwa Allah, mtii kamili, wala hakuwa miongoni mwa washirikina. (Alikuwa)mwenye kuzishukuru neema zake (Mwenyezi Mungu zilizo juu yake) Akamchagua na kumuongoza katika njia iliyonyooka. Na tukampa wema katika dunia na hakika yeye katika Akhera atakuwa miongoni mwa washirikina. Kisha tukakufunulia ya kwamba ufuate* ***mila (Dini) ya Ibrahiim (aliyekuwa) mtii kamili, wala*** *hakuwa miongoni mwa washirikina” (16:120-123).*

وَمَنْ أَحْسَنُ دِينًا مِّمَّنْ أَسْلَمَ وَجْهَهُۥ لِلَّهِ وَهُوَ مُحْسِنٌ وَٱتَّبَعَ مِلَّةَ إِبْرَٰهِيمَ

حَنِيفًا ۗ وَٱتَّخَذَ ٱللَّهُ إِبْرَٰهِيمَ خَلِيلًا ﴿١٢٥﴾

*"Na nani aliye bora kwa Dini kuliko yule ambaye ameuelekeza uso wake kwa Allah, naye ni mtendaji mema (mwema) na anafuata* ***mila ya Ibrahim*** *Na Allah amemfanya Ibrahim kuwa ni kipenzi chake' (4:125).*

- Mwenyezi Mungu alipomuamrisha Mtume Muhammad (s.a.w) kuwa afuate **mila ya Ibrahiim(a.s) alikuwa na maana hiyo.**
- **Kwani mila ya Ibrahim** kulingana na aya tulizozirejea ni kuwa Muislamu ni mtu ajisalimishaye kwa kila lake katika kufuata amri za Mola wake Muumba.

- Mila yenyewe ya Ibrahiim(a.s) aliyowausia wanawe kuifuata inaaainishwa katika aya zifuatazo:

إِذۡ قَالَ لَهُۥ رَبُّهُۥٓ أَسۡلِمۡۖ قَالَ أَسۡلَمۡتُ لِرَبِّ ٱلۡعَٰلَمِينَ ١٣١ وَوَصَّىٰ بِهَآ

إِبۡرَٰهِـۧمُ بَنِيهِ وَيَعۡقُوبُ يَٰبَنِيَّ إِنَّ ٱللَّهَ ٱصۡطَفَىٰ لَكُمُ ٱلدِّينَ فَلَا تَمُوتُنَّ إِلَّا

وَأَنتُم مُّسۡلِمُونَ ١٣٢

*“(Kumbukeni habari hizi) Mola wake (Ibrahim) alipomwambia silimu (jisalimishe), akasema, “Nimejisalimisha kwa Mola wa walimwengu wote”. Na Ibrahim akawausia haya wananawe, na Yakubu (pia akawausia wanawe) “Enyi wanangu Hakika Mwenyezi Mungu amekuchagulieni Dini hii (ambayo ndiyo mila yangu) basi msife ila nanyi mmekuwa wenye kujisalimisha: (2:131-132).*

- Wataalamu wa fani ya **sayansi ya jamii wanatafsiri neno culture (mila)** kuwa ni:

*"A whole way of life, material, intellectual and spiritual of a people".*

Tafsiri:

*"Ni njia kamili ya maisha ya kimwili,kiakili na kiroho"*

- **Ukirejea katika Qur'an utakuta vile vile neno "Dini" limetumika kama siku ya malipo, yaani mfumo wa maisha ya Akhera. Hebu turejee aya chache** zifuatazo:

مَـٰلِكِ يَوْمِ ٱلدِّينِ ﴿٤﴾

*"Mwenye kumiliki siku ya (Dini) malipo" (1:4).*

أَرَءَيْتَ ٱلَّذِى يُكَذِّبُ بِٱلدِّينِ ﴿١﴾

*“Je umemuona yule anayekadhibisha “Dini” (anayekabidhisha maisha ya Akhera?”) (107:1).*

فَمَا يُكَذِّبُكَ بَعْدُ بِٱلدِّينِ ﴿٧﴾ أَلَيْسَ ٱللَّهُ بِأَحْكَمِ ٱلْحَٰكِمِينَ ﴿٨﴾

*“Basi ni lipi likupalo, kukadhibisha Dini (maisha ya akhera) baada (ya kuona hayo?). Je, Allah si Hakimu maudilifu kuliko mahakimu wote?” (95:7-8).*

Hata katika maana hii, neno Dini pia halikutumiwa kwa maana finyu bali limetumika kwa maana ya mfumo mzima wa maisha ya akhera ambapo Allah(s.w) atakuwa ndiye mfalme pekee na kila mtu atahukumiwa na kulipwa kwa uadilifu kutokana na amali (matendo) zake alizochuma katika mfumo wa maisha wa hapa duniani.

- Kutokana na aya za Qur’an tulizozirejea, tunajifunza kwa ujumla kuwa “Dini” ni mfumo wowote wa maisha anaoufuata mwanaadamu katika kuendesha maisha yake ya binafsi na jamii katika nyanja zote za maisha.
- Kuna Dini (mifumo) nyingi. Lakini kwa urahisi tunaweza kuzigawanya “Dini” katika makundi mawili makubwa:

(i) Dini ya Allah(s.w).
(ii) Dini za watu.

- Dini ya Allah(s.w) ni mfumo wa maisha ya mwanaadamu unaofuata muongozo wa Allah(s.w).
- Dini ya Allah ni maarufu kwa jina la **Al-Islam.**

- Dini za watu ni mifumo ya maisha iliyowekwa na Wanaadamu kutokana na matashi yao.
- Dini za watu ni nyingi lakini nazo tunaweza kuzigawanya katika makundi makubwa matatu yafuatayo:

(a) **Dini ya Ukafiri; ni utaratibu uliofumwa juu ya misingi ya** kukanusha muongozo wa Allah(s.w) na Mitume wake.

(b) **Dini ya Ushirikina; ni utaratibu wa maisha uliofumwa juu ya** misingi ya kumshirikisha Allah(s.w) na miungu wengine waliyobuni wanaadamu wenyewe.

(c) **Dini ya Utawa; ni utaratibu ambao wafuasi wake hujitenga mbali** na harakati za kumletea mwanaadamu maendeleo ya hapa ulimwenguni. Watawa hujizuilia vyakula na vinywaji vizuri na halali, hujizuia kuvaa nguo nzuri, kuishi katika nyumba nzuri na kujizuilia na vile vyote vitakavyowaletea burudisho na furaha ya kimwili. Watawa wamebuni mfumo huu wa maisha kutokana na kutolielewa vema lengo la maisha ya mwanaadamu hapa ulimwenguni na kutoelewa kwao maana halisi ya ibada kwa mtazamo wa Uislamu.

- Katika Dini zote hizi, Dini anayoiridhia Allah(s.w) ni moja tu nayo ni **Al-Islam (Uislamu) kama inavyobainika katika Qur'an:**

إِنَّ ٱلدِّينَ عِندَ ٱللَّهِ ٱلْإِسْلَٰمُ

*"Bila shaka Dini (ya haki) mbele ya Allah ni Al-Islam (Uislamu)..." (3:19).*

وَمَن يَبْتَغِ غَيْرَ ٱلْإِسْلَٰمِ دِينًا فَلَن يُقْبَلَ مِنْهُ وَهُوَ فِى ٱلْءَاخِرَةِ مِنَ

ٱلْخَٰسِرِينَ ﴿٨٥﴾

*“Na anayetaka Dini nyingine isiyokuwa ya Al-Islam (ya Uislamu) basi hatakubaliwa kwake. Naye katika Akhera atakuwa ni miongoni mwa wenye khasara.”(3:85).*

# Maana ya Al-Islam

- Al-Islam(Uislamu) ni jina la Dini ya Allah (s.w).

***Islam ni neno la*** Kiarabu lenye maana zifuatazo:

# Maana ya kwanza ya Islam

- Mwenendo mwema au kujisalimisha moja kwa moja au kutii kwa unyenyekevu.

Kutokana na maana hii, ***Al-Islam ni Dini ya kutenda mema*** na kuacha maovu kwa kufuata bara bara sheria za Muumba.

- Kwa maana nyingine Uislamu ni utaratibu wa maisha unaofuata bara bara mwongozo wa Allah(s.w) na Sunnah ya Mitume wake.
- Hivyo wale wote wanaojiepusha na maovu na wakatenda mema kwa mujibu wa maelekezo ya Muumba wao na kufuata sunnah za Mitume ni waislamu.

**Al-Islam kwa maana hii ya kwanza ya kutii kwa unyenyekevu sheria za** Muumba, inatupa funzo kuwa mimea, wanyama, na viumbe vyote vilivyomo mbinguni na ardhini vinafuata Uislamu kwa sababu vinafuata barabara sheria za maumbile (Natural Laws) alizoziweka Muumba. Allah(s.w) anatutanabahisha katika Qur’an:

أَفَغَيْرَ دِينِ ٱللَّهِ يَبْغُونَ وَلَهُۥٓ أَسْلَمَ مَن فِى ٱلسَّمَـٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ طَوْعًا

وَكَرْهًا وَإِلَيْهِ يُرْجَعُونَ ﴿٨٣﴾

*"Je wanataka Dini isiyokuwa ya Allah na hali kila kilichomo mbinguni na ardhini, kimejisalimisha kwake (kina mtii yeye) kipende kisipende? Na kwake watarejeshwa wote". (3:83).*

- Ni kweli kuwa kila kiumbe kinamtii Allah(s.w) kwa kufuata sheria za maumbile za kibaiolojia (Biological Laws), kikemia (Chemical Laws) na za Kifizikia (Physical Laws) ambazo zimefungamana na maumbile ya kila kiumbe. Kwa mantiki hii, mwili wa mwanaadamu nao hauna hiari ya kutotii sheria za maumbile.

➢Hivyo mwili wa mwanaadamu nao ni "Muislamu" yaani unafuata sheria za maumbile, upende usipende. Allah(s.w) anatufahamisha hili:

فَأَقِمْ وَجْهَكَ لِلدِّينِ حَنِيفًا ۚ فِطْرَتَ ٱللَّهِ ٱلَّتِى فَطَرَ ٱلنَّاسَ عَلَيْهَا ۚ لَا
تَبْدِيلَ لِخَلْقِ ٱللَّهِ ۚ ذَٰلِكَ ٱلدِّينُ ٱلْقَيِّمُ وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَ ٱلنَّاسِ لَا
يَعْلَمُونَ ﴿٣٠﴾

*“Basi uelekeze uso wako katika Dini iliyo sawasawa. Ndilo umbile Allah alilowaumbia watu (yaani Dini ya Al-Islam inawafikiana barabara na umbo la binaadamu). Hakuna mabadiliko katika maumbile ya viumbe vya Allah. Hiyo ndiyo Dini ya haki, lakini watu wengi hawajui” (30:30).*

**Maana ya pili ya Islam.**

Pia neno “***Islam” linatokana na neno “salama” lenye maana ya*** amani. Kwa maana hii Al-Islam ni Dini ya amani. Kwa maana nyingine utaratibu wa maisha unaoendeshwa kwa kujisalimisha kwa Allah(s.w) kwa kufuata kwa ukamilifu sheria za Allah(s.w), ndio pekee unaoweza kuleta furaha na amani ya kweli kwa mtu binafsi na kwa jamii nzima kwa ujumla.

# Nani Muislamu

Kutokana na maana ya kwanza ya “**Al-Islam”, Muislamu ni yule** anayemnyenyekea Allah(s.w) kwa kufuata kwa ukamilifu sheria zake zote. Kwa maana nyingine Muislamu wa kweli ni yule anayeishi kwa kuchunga mipaka ya Allah(s.w) kwa kufanya yale yote aliyomuamrisha na kuacha yale yote aliyomkataza katika maisha yake ya kila siku ya kibinafsi na kijamii.

➢Allah(s.w) anawahimiza waumini wa kweli wafuate kwa ukamilifu sheria zake zote katika maisha yao yote:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ ٱدْخُلُوا۟ فِى ٱلسِّلْمِ كَآفَّةً وَلَا تَتَّبِعُوا۟ خُطُوَٰتِ
ٱلشَّيْطَٰنِ ۚ إِنَّهُۥ لَكُمْ عَدُوٌّ مُّبِينٌ ﴿٢٠٨﴾

*“Enyi Mlioamini! Ingieni kwa ukamilifu katika Uislamu wala msifuate nyayo za shetani. Kwa hakika yeye kwenu ni adui dhahiri” (2:208).*

Pia Allah(s.w) anawaamrisha waumini:

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ ٱتَّقُوا۟ ٱللَّهَ حَقَّ تُقَاتِهِۦ وَلَا تَمُوتُنَّ إِلَّا وَأَنتُم مُّسْلِمُونَ ﴿١٠٢﴾

*“Enyi Mlioamini! Mcheni Allah kama ipasavyo kumcha wala msife isipokuwa mmekwisha kuwa Waislamu kamili” (3:102).*

- Mtu asiyeishi kwa kumtii Allah(s.w) kwa kufuata maamrisho yake yote na kuacha makatazo yake si Muislamu wa kweli hata kama atadai kuwa ni Muislamu na akaitwa jina la Kiislamu.

# Zoezi la 1:2

1. (a) Maana ya Dini kwa Mtazamo wa Makafiri ni ____
(b) Maana ya Dini kwa Mtazamo wa Uislamu ni ______
2. Hapa Ulimwenguni kuna Dini kubwa mbili ambazo ni:-
(a) ____________________
(b) ____________________
3. *"Je, Wanataka Dini isiyokuwa ya Mwenyezi Mungu na hali kila kilichomo mbinguni na ardhini kimejisalimisha kwake kipende kisipende. Na kwake Mtarejeshwa wote" (3:83).*
Kwa kuzingatia aya hii toa mafunzo mawili (2) yanayohusiana na Dini.

4. (a) Toa maana mbili za neno “Islam”.

(b) Nani Muislamu?

# *Sura ya Pili*

# FIQH

- Katika kitabu hiki somo la Fiqh litazingatia mada kuu zifuatazo:
  - Fani ya Fiqh.
  - Mtazamo wa Uislamu juu ya Ibada.
  - Shahada.
  - Kusimamisha Swala.
  - Vipengele vya Tabia njema.

# FANI YA FIQH

## Maana ya Fiqh

- Fiqh ni fani ya Elimu ya Kiislamu inayohusiana na ufahamu juu ya maamrisho na makatazo ya mambo mbalimbali ya kibinafsi na kijamii.
- Baadhi ya Wanazuoni wa Kiislamu wamefasiri Fiqh kama ni taaluma ya sharia ya Kiislamu au ni maarifa ya hukumu za Kiislamu (Islamic jurisprudence) zitokanazo na Qur’an na Sunnah ili kutoa maongozi kwa mtu binafsi na jamii.

- Mara nyingi maneno “***Fiqh” na “Sheria” yamekuwa yakitumiwa kwa*** maana moja, hata hivyo yanatofautiana kidogo katika tafsiri.
- Fiqh ni maarifa juu ya hukumu mbalimbali za Kiislamu au ni wa utekelezeji wa sheria za Kiislamu.
- Na ***Sharia ni maamrisho na makatazo yaliyomo ndani*** ya Qur’an:

ثُمَّ جَعَلْنَـٰكَ عَلَىٰ شَرِيعَةٍ مِّنَ ٱلْأَمْرِ فَٱتَّبِعْهَا وَلَا تَتَّبِعْ أَهْوَآءَ ٱلَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ ﴿١٨﴾

*"Kisha tumekuwekea katika sharia (itokanayo) na amri yetu, basi ufuate wala usifuate matamanio ya wale wasiojua (kitu) (45:18).*

- Kwa hiyo sheria ni ufunuo juu ya masuala mbalimbali, uliomo ndani ya Qur'an na Sunnah, Fiqh ni ufafanuzi wa utekelezaji wa sheria hasa katika mas-ala ambayo hayako wazi.

# Matapo ya Fiqh

Fiqh imegawanyika katika matapo mawili:
(i) Fiqh ya matendo mahsusi au ya Ibada maalumu ya muumini kama vile Swalat, Funga, Zakat na Hija, n.k.
(ii) Fiqh ya masuala mbalimbali ya kijamii (Muamalaat), mathalan, sheria za mahusiano ya kifamilia (ndoa, talaka na eda, mirathi, uzazi), sheria za mahusiano ya jamii – sheria za mahakama, sheria za usalama wa maisha na mali, utaratibu wa kuchuma na biashara, Benki, kanuni za vita (2:190), mahusiano ya kijamii; mahusiano ya kimataifa, siasa na uendeshaji wa dola,n.k.

# Misingi ya Fiqh

- Muundo wa Fiqh umesimama juu ya misingi mitatu

**(i) Qur’an**

Qur’an ndio chem.-chem ya sheria kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

وَكَذَٰلِكَ أَنزَلْنَٰهُ حُكْمًا عَرَبِيًّا ۚ وَلَئِنِ ٱتَّبَعْتَ أَهْوَآءَهُم بَعْدَمَا جَآءَكَ مِنَ
ٱلْعِلْمِ مَا لَكَ مِنَ ٱللَّهِ مِن وَلِىٍّ وَلَا وَاقٍ ﴿٣٧﴾

*“Na namna hii tumeiteremsha (hii Qur’an) hali ya kuwa ni Hukumu (ya Mwenyezi Mungu iliyoteremka) kwa (lugha ya) Kiarabu. Na kama ukifuata matamanio yao baada ya kukufikia elimu hii, hutakuwa na rafiki wala mlinzi mbele ya Mwenyezi Mungu” (13:37).*

يَمۡحُواْ ٱللَّهُ مَا يَشَآءُ وَيُثۡبِتُۖ وَعِندَهُۥٓ أُمُّ ٱلۡكِتَٰبِ ٣٩

*"Mwenyezi Mungu hufanya ayatakayo na huthubutisha (ayatakayo) na asili ya Hukumu zote iko kwake (Mwenyezi Mungu)"" (13:39).*

- Kwa muktadha huu Allah(s.w) anatuamrisha kumtii Mtume(s.a.w) na kumfanya kiigizo cha maisha yetu:

قُلْ إِن كُنتُمْ تُحِبُّونَ ٱللَّهَ فَٱتَّبِعُونِى يُحْبِبْكُمُ ٱللَّهُ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ ۗ
وَٱللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٣١﴾ قُلْ أَطِيعُوا۟ ٱللَّهَ وَٱلرَّسُولَ ۖ فَإِن تَوَلَّوْا۟ فَإِنَّ ٱللَّهَ
لَا يُحِبُّ ٱلْكَٰفِرِينَ ﴿٣٢﴾

*Sema:“Ikiwa nyinyi mnampenda Mwenyezi Mungu,basi nifuateni;(hapo)Mwenyezi Mungu atakupendeni na atakughufirieni madhambi yenu. na Mwenyezi Mungu ni mwenye maghufira (na) mwenye rehema. Sema:”Mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume (wake). Na kama mkikengeuka, (Mwenyezi Mungu atakutieni adabu), kwani Mwenyezi Mungu hawapendi makafiri.(3:31-32)*

لَّقَدۡ كَانَ لَكُمۡ فِي رَسُولِ ٱللَّهِ أُسۡوَةٌ حَسَنَةٞ لِّمَن كَانَ يَرۡجُواْ ٱللَّهَ وَٱلۡيَوۡمَ
ٱلۡأٓخِرَ وَذَكَرَ ٱللَّهَ كَثِيرٗا ٢١

*"Bila shaka mnao mfano mwema (ruwaza nzuri)kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, kwa mwenye kumuogopa Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho, na kumtaja Mwenyezi Mungu sana". (33:21)*

وَمَآ ءَاتَىٰكُمُ ٱلرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا نَهَىٰكُمۡ عَنۡهُ فَٱنتَهُواْ

*"na anachokupeni Mtume basi pokeeni, na anachokukatazeni jiepusheni nacho. (59:7)*

**(iii) Ijtihad**

- *Ijtihad* ni jitihada waliyoifanya maswahaba wa mtume na mujtahidi wengine katika ufafanuzi wa tafsiri ya Sheria zilizomo katika Qur’an na Hadith (Sunnah) za Mtume (s.a.w) kwa misingi ya “Qiyas” na “Ijmaa”.
- Qiyas – maana yake ni kupima, na madhumuni yake ni kuchunguza msingi wa sheria ili iweze kushughulikia masuala mengi.
- Ni utaratibu wa kujua (tafsiri ya) sheria zilizomo ndani ya Qur’an na Hadith Sahihi (Sunnah) ili kuyapatia ufumbuzi (hukumu) masuala mbalimbali.

# Ijmaa

(consensus) – maana yake ni maafikiano ya Mujitahidina katika ufafanuzi wa hukumu ya jambo fulani kwa mnasaba wa Qur’an au Hadith (Sunnah) za Mtume (s.a.w). Kimsingi, Ijmaa hutumika pale Waislamu wanapotakiwa kutoa hukumu ya jambo fulani ambalo hukumu yake haikowazi katika Qur’an, hata hivyo, zoezi hilo hufanyika kwa kuzingatia Qur’an na Hadith Sahihi(Sunnah).

- Kwa misingi hiyo yaani **Qur'an, Hadith, Qiyas na Ijmaa (Usul al-**Fiqh), katika Uislamu hakuna mabadiliko ya sheria kulingana na wakati.
- Sheria ni zile zile zilizomo ndani ya Qur'an na Hadith (Sunnah), kinachohitajika ni ufafanuzi na utekelezaji kwa mujibu wa mazingira.

- Ijmaa haina ukomo wa zama au nchi. Hivyo fikra kuwa walioafikiana wanazuoni wa zama fulani ndilo linalopaswa kufuatwa zama zote si fikra sahihi.
- Wakati wa uhai wa Mtume (s.a.w) Maswahaba hawakufanya Ijtihada kwa sababu Mtume alikua akitoa ufumbuzi wa suala lolote lililojitokeza, hii ikiwa ni pamoja na kushushiwa Wahyi.

- Lakini baada ya kutawafu Mtume(s.a.w) Maswahaba zake walilazimika kupanua tafsiri ya vipengele mbalimbali.
- Katika zoezi la ufafanuzi wa tafsiri ya sheria zilizomo katika Qur'an na Hadith, Maswahaba walitumia misingi ya **Qiyas** na **Ijmaa (muafaka).44**

- Jambo la awali kabisa lililowatatiza Maswahaba lilikuwa ni uchaguzi wa Khalifa wa kwanza Abubakar(r.a).
- Kwa kuzingatia kuteuliwa kwake na Mtume(s.a.w) kuongoza sala ya Jamaa, Maswahaba wakafikia uamuzi wa pamoja wa kumchagua Abubakar(r.a) awe Amir/Kiongozi wao katika mambo yote.
- Kwa msingi wa Qiyas kuwa, Imam wa Swala ndio huyo huyo awe kiongozi wa dola.

- Hukumu ya Mtume(s.a.w) hapa imetafsiriwa kwa upana kutatua kitendawili cha nani awe Khalifa.
- Hivyo uchaguzi wa Khalifa wa kwanza ulifanywa kwa msingi wa **Qiyas na maswahaba** waliafikiana(**Ijmaa).**
- **Hali kadhalika, kwa msingi huo wa Qiyas,** maswahaba walitafsiri sheria nyingine nyingi na kuyapatia ufumbuzi maswala mengi na ya aina mbalimbali.

- Kwa kigezo cha uchaguzi wa Khalifa wa kwanza – Abubakar(r.a), ambao ulifanyika kwa misingi yote miwili ya **Qiyas na Ijmaa, utaratibu** huo ulijumuishwa katika misingi ya sheria ya Kiislamu lakini ikiwa chini ya misingi mikuu ya awali **Qur’an na Sunnah.**
- **Hivyo misingi hiyo** imepangika kama ifuatavyo:

(i) Qur’an
(ii) Hadith (Sunnah)
(iii) Qiyas na Ijmaa(Ijtihad).

- Katika taaluma ya Fiqh kanuni hizi za msingi huitwa **Usul-al-Fiqh** (foundamental principles).

# MTAZAMO WA UISLAMU JUU YA IBADA

## Maana ya Ibada

Neno "*Ibada" limetokana na neno la Kiarabu "Abd" lenye maana ya* mtumwa au mja. Hivyo neno "Ibada" lina maana ya kutumikia. Kufanya "Ibada" au Kumuabudu Mwenyezi Mungu ni kumtumikia Mwenyezi Mungu kwa kumtii kwa unyenyekevu kwa kufuata maamrisho yake na kuacha makatazo yake yote.

- Tunafahamishwa katika Qur’an kuwa lengo la kuumbwa Mwanaadamu na kuletwa hapa ulimwenguni ni kumuabudu Mwenyezi Mungu.

وَمَا خَلَقْتُ ٱلْجِنَّ وَٱلْإِنسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ ٥٦

*“Sikuwaumba majini na watu ila wapate kuniabudu” (51:56).*

- Kutokana na aya hii tunajifunza kuwa mwanaadamu ameletwa hapa duniani ili amuabudu Mwenyezi Mungu katika maisha yake yote.
- Ni vipi mtu ataweza kumuabudu Mwenyezi Mungu kwa kumtii kwa unyenyekevu katika kila jambo analolifanya katika kila hatua na kila kipengele cha maisha yake ya kibinafsi na kijamii ?

- Ni kumtii Mwenyezi Mungu kwa unyenyekevu katika kila jambo mtu analolifanya au kufanya kila jambo kwa kufuata barabara mwongozo wa Mwenyezi Mungu ulio wazi katika vitabu vyake na Sunnah za Mtume wake ikiwa ni pamoja na kuchunga mipaka ya halali na haramu iliyobainishwa katika mwongozo huo.

- Hivyo chochote kile atakachokifanya mja chenye manufaa kwake binafsi au kwa jamii kwa ujumla kwa matarajio ya kupata radhi ya Mwenyezi Mungu na akawa amelifanya kwa kufuata barabara mwongozo wa Mwenyezi Mungu kitakuwa ni kitendo cha “Ibada” mbele ya Mwenyezi Mungu.

- Kwa mfano mtu anapojiingiza katika harakati za uchumi akawa anazingatia mwongozo wa Mwenyezi Mungu kwa lengo la kujipatia riziki ya halali na kupata mali ya kupigania Dini ya Mwenyezi Mungu huwa yumo katika (ibada).
- Kila jambo analolifanya mja kwa mtazamo huu ni ibada kama tunavyojifunza katika Hadith zifuatazo:

*Jabir na Hudhaifa (r.a) wameeleza kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: “Kila kitendo kizuri ni sadaqa” (Al-Bukhari na Muslim).*

- Katika Hadith iliyosimuliwa na Abu Hurairah(r.a), Mtume(s.a.w) amesema:

*“Katika kila kiungo cha mwili kuna sadaqa. Kuna sadaqa katika kila kitu, kufanya uadilifu kati ya watu wawili ni sadaqa; kumsaidia mtu kumpanda mnyama wake anayesafiri naye au kumtwika mtu mzigo wake ni sadaqa; neno zuri ni sadaqa; na kila hatua mtu anayotembea kwenda kwenye swala ni sadaqa, na kuondoa kitu kibaya njiani ni sadaqa” (Al-Bukhari na Muslim).*

- Neno “Sadaqa” kama ilivyotumika katika Hadith hizi lina maana ya tendo zuri analolifanya mtu kumfanyia mtu mwingine au kuifanyia nafsi yake.

# Nguzo za Uislamu

- Nguzo za Uislamu zimebainishwa katika Hadith ifuatavyo:

*Ibn Umar (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: "Uislamu umejengwa juu ya nguzo tano: Kushuhudia kuwa hapana Mola ila Mweneyzi Mungu na kushuhudia kuwa Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu Kusimamisha Swala, kutoa Zaka, Kufunga Ramadhani na Kuhiji Makkah kwa wenye uwezo" (Al-Bukhari na Muslim).*

- Kutokana na Hadith hii tunajifunza kuwa nguzo za Uislamu ni tano:

(1) Kutoa Shahada mbili kwa kushuhudia kuwa hapana Mola ila Mwenyezi Mungu na kushuhudia kuwa Muhammad ni Mtume
wa Mwenyezi Mungu.

(2) Kusimamisha swala.

(3) Kufunga mwezi wa Ramadhani.

(4) Kutoa Zakat.

(5) Kuhiji Makkah kwa mwenye uwezo.

- Baadhi ya Waislamu wameihusisha “Ibada” na utekelezaji tu wa hizi nguzo za Uislamu na Sunnah zinazoambatana nazo kama vile swala za Sunnah, funga za Sunnah, utoaji wa sadaqa, kufanya “Umrah” n.k.
- Kwa mtazamo wao huu Uislamu wa mtu unaweza kukamilika kwa kutekeleza tu hizi nguzo za Uislamu.
- Kwa maana nyingine Muislamu mwenye mtazamo huu akitekeleza tu nguzo tano za Uislamu atakuwa ameshatekeleza lengo la kuumbwa kwake.

- Ukizingatia kwa makini utaona kuwa mtazamo huu wa Ibada si sahihi kwani muda tunaotumia katika kutekeleza hizi ibada za Swala, Zakat, Swaumu, n.k. ni mdogo sana ukilinganisha na utendaji wetu wa kila siku.
- Kwa mfano muda tunaotumia katika kusimamisha swala tano za siku ni saa moja tu hivi, yaani 1/24 ya siku, zakat tunatoa 21/2 % ya mali baada ya kupindukia mwaka tena kwa walio matajiri tu;

- Tunafunga mwezi mmoja tu kwa mwaka tena kwa masaa machache kati ya saa 13 na 14 kwa watu wa nchi za joto (tropical lands) na Hija ni mara moja katika umri wa mtu.
- Ni muhali kwa Mwenyezi Mungu Mjuzi mwenye Hekima atangaze kuwa “Sikuwaumba majini na watu ila wapate kuniabudu”.

- Kumuabudu kwenyewe kuishie kwenye utekelezaji wa nguzo tano tu za Uislamu ambazo huchukua sehemu ndogo sana ya maisha ya mwanaadamu.
- Bila shaka tangazo hilo la Mwenyezi Mungu lina maana kuwa mwanaadamu ili atekeleze lengo la kuumbwa kwake, hana budi kumuabudu Mwenyezi Mungu kwa saa zote 24 za maisha yake ya kila siku kwa umri wake wote.
- Hivi ndivyo anavyo sisitiza Allah(s.w) katika aya zifuatazo:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ ٱدۡخُلُواْ فِي ٱلسِّلۡمِ كَآفَّةٗ وَلَا تَتَّبِعُواْ

خُطُوَٰتِ ٱلشَّيۡطَٰنِۚ إِنَّهُۥ لَكُمۡ عَدُوّٞ مُّبِينٞ ٢٠٨

*"Enyi mlioamini! Ingieni katika hukumu za Uislaamu zote,wala msifuate nyayo za shetani; kwa hakika yeye kwenu ni adui dhahiri" (2:208)*

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ ٱتَّقُوا۟ ٱللَّهَ حَقَّ تُقَاتِهِۦ وَلَا تَمُوتُنَّ إِلَّا وَأَنتُم

مُّسْلِمُونَ ﴿١٠٢﴾

*"Enyi mliamini! Mcheni Mwenyezi Mungu kama ipasavyo kumcha; wala msife isipokuwa mmekwishakuwa Waislamu kamili'.(3:102)*

وَٱعْبُدْ رَبَّكَ حَتَّىٰ يَأْتِيَكَ ٱلْيَقِينُ ﴿٩٩﴾

*"Na umuabudu Mola wako mpaka ikufikie hiyo yakini(Nayo ni umauti"(15:99)*

- Pia aya zifuatazo zinatufahamisha kuwa mwanaadamu mwenye akili ni yule anayemuabudu Allah(s.w) saa 24.

إِنَّ فِي خَلْقِ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ وَٱخْتِلَٰفِ ٱلَّيْلِ وَٱلنَّهَارِ لَءَايَٰتٍ لِّأُوْلِي
ٱلْأَلْبَٰبِ ١٩٠ ٱلَّذِينَ يَذْكُرُونَ ٱللَّهَ قِيَٰمًا وَقُعُودًا وَعَلَىٰ جُنُوبِهِمْ
وَيَتَفَكَّرُونَ فِي خَلْقِ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ رَبَّنَا مَا خَلَقْتَ هَٰذَا بَٰطِلًا
سُبْحَٰنَكَ فَقِنَا عَذَابَ ٱلنَّارِ ١٩١

*“Katika kuumbwa mbingu na ardhi na mfuatano wa usiku na mchana, ziko hoja zakuonyesha kuwepo Mwenyezi Mungu Mmoja),kwa wenye akili. Ambao humkumbuka Mwenyezi Mungu wakiwa wima na wakikaa na wakilala. Na huzingatia umbo la mbingu na ardhi (Pia. ‘Namna gani Mwenyezi Mungu alivyoumba. Wasema: ”Mola wetu; ! Hukuviumba hivi bure. Utukufu ni wako Basi tuepushe na adhabu ya moto”.(3:190 - 191)*

- Tukirejea kwenye Hadith ya Ibn Umar (r.a) tunafahamishwa juu ya nguzo za Uislamu.
- Hadith hiyo imetufahamisha kuwa “Uislamu umejengwa juu ya nguzo tano” na sio “Uislamu ni nguzo tano”. Ukichukua mfano nyumba iliyosimamishwa na “nguzo tano’ huwezi kuhamia nyumba hiyo kwa kusimamishwa nguzo tano tu.

- Bali ni lazima yafanywe mambo mengine kama vile kuzungusha ukuta, kuweka paa, madirisha, milango, sakafu, na mengineyo yanayofikisha nyumba kwenye ukamilifu.
- Kwa mfano huu wa nyumba, tunajifunza kuwa nguzo za Uislamu ni msingi au nguzo za kusimamisha Uislamu.
- Bila ya nguzo tano Uislamu hauwezi kusimama.
- Lakini Uislamu haukamiliki kwa kusimamisha nguzo tano tu.

# Lengo la Nguzo za Uislamu

- Lengo hasa la Waislamu kuamrishwa kusimamamisha nguzo tano za Uislamu ni ili kuwaandaa waweze kumuabudu Mwenyezi Mungu katika kila kipengele cha maisha yao yote.
- Kila nguzo katika hizi tano imekusudiwa imuandae Muislamu katika uwanja maalum ili hatimaye baada ya kutekeleza nguzo zote kwa pamoja afikie lengo la maisha yake.
- Hebu turejee kwa muhtasari lengo maalum la kila nguzo ya Uislamu:

# (1) Shahada mbili

- Shahada ndio kiingilio na kitambulisho cha Muislamu kwa Umma wa Kiislamu.
- Shahada ni ahadi anayotoa mja mbele ya Mola wake na Mbele ya walimwengu wote kuwa atamtii Allah(s.w) na Mtume wake katika kuendea kila kipengele cha maisha yake yote.
- Kwa kujikumbusha ahadi hii ya shahada kila mara na hasa kila anaposikia katika adhana na kuirejea katika swala, humfanya mja abakie katika utii wa Allah(s.w) na Mtume wake katika utendaji wake wa saa 24 katika maisha yake yote.

# (2) Kusimamisha Swala

- Humtayarisha mja kujizuilia na mambo maovu na machafu kama tunavyofahamishwa katika Qur’an:

ٱتْلُ مَآ أُوحِىَ إِلَيْكَ مِنَ ٱلْكِتَٰبِ وَأَقِمِ ٱلصَّلَوٰةَ ۖ إِنَّ ٱلصَّلَوٰةَ
تَنْهَىٰ عَنِ ٱلْفَحْشَآءِ وَٱلْمُنكَرِ ۗ وَلَذِكْرُ ٱللَّهِ أَكْبَرُ ۗ وَٱللَّهُ يَعْلَمُ مَا
تَصْنَعُونَ ﴿٤٥﴾

*“Soma uliyoletewa Wahyi(uliyofunuliwa) katika kitabu (hiki) na usimamishe swala. Hakika ya Swala (ikiswaliwa vilivyo) humzuiliya (huyo mwenye kuswali) na mambo machafu na maovu, na kwa yakini kumbuko la Mwenyezi Mungu (lililomo ndani ya Swala) ni jambo kubwa kabisa (la kumzuilia mtu na mabaya) Mwenyezi Mungu anayajua mnayoyatenda” (29:45).*

- Hivyo lengo la swala ni kumtakasa mja na kumkinga na mambo maovu na machafu.

# (3) Zakat

- Imekusudiwa kuitakasa nafsi ya mtoaji kutokana na maasi yanayosababishwa na suala la umilikaji wa mali kama vile, uchumi haramu, husuda, upupiaji wa mali, dhulma, ubakhili, ufujaji mali, n.k.
- Kwa upande mwingine utoaji wa Zakat katika jamii huitakasa jamii kwa kujenga hali ya kuhurumiana, kupendana, kushirikiana na kushikamana kama mwili mmoja.
- Lengo la utoaji wa Zakat na Sadaqat linabainishwa katika aya ifuatayo:

خُذْ مِنْ أَمْوَٰلِهِمْ صَدَقَةً تُطَهِّرُهُمْ وَتُزَكِّيهِم بِهَا وَصَلِّ عَلَيْهِمْ ۖ إِنَّ صَلَوٰتَكَ سَكَنٌ لَّهُمْ ۗ وَٱللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿١٠٣﴾

*"Chukua sadaka katika mali zao, uwasafishe na kuwatakasa kwa ajili ya hizo (sadaqa zao) na kuwataja kwa vizuri (mbele yangu) na uwaombee dua. Hakika kuwaombea kwako kutawapa utulivu (watengenekewe) na Mwenyezi Mungu ndiye asikiaye na ajuaye" (9:103).*

# (4) Swaumu

- Humuandaa mja kuwa Mcha-Mungu. Mcha Mungu ni yule anayemtii Allah(s.w) ipasavyo kwa kufuata maamrisho yake yote na kuacha makatazo yake yote.
- Kwa maana nyingine Ucha-Mungu ni kuishi kwa kuchunga barabara mipaka ya Allah(s.w) aliyowawekea wanaadamu katika kukiendea kila kipengele cha maisha yao ya kila siku.

- Lengo hili la Swaumu limebainsihwa katika aya ifuatayo:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ كُتِبَ عَلَيۡكُمُ ٱلصِّيَامُ كَمَا كُتِبَ عَلَى ٱلَّذِينَ مِن
قَبۡلِكُمۡ لَعَلَّكُمۡ تَتَّقُونَ ١٨٣

*“Enyi Mlioamini! Mmelazimishwa kufunga (Swaumu) kama walivyolazimishwa waliokuwa kabla yenu ili mpate kumcha Mwenyezi Mungu” (2:183).*

# (5) Hija

- Humtayarisha mja kumpenda Allah(s.w) kuliko chochote katika ulimwengu hata kuliko nafsi yake.
- Humfanya mja atumie mali yake na afunge safari ndefu yenye taabu na mashaka, aiache familia yake na wapenzi wake wengine kwa ajili tu ya kuitikia wito wa Allah(s.w).
- Pia Hija huwatayarisha watu kujenga usawa, udugu na umoja wa kweli.

- Walimwengu wote wanaohudhuria kwenye Hija huvaa vazi moja (ihram), hukaa pamoja na kufanya ibada mbalimbali pamoja bila kujali tofauti zao za rangi, taifa, hadhi, n.k.
- Miongoni mwa matendo ya Hija ni yale ya kuwatayarisha waja kuwa Askari wa Allah(s.w) walio tayari kupigania Dini yake kwa mali zao na nafsi zao.

- Hivyo, kwa vyovyote vile, hizi nguzo tano zikisimamishwa ipasavyo zitawawezesha Waislamu kusimamisha Uislamu katika jamii na kuwa Makhalifa wa Mwenyezi Mungu(s.w) hapa limwenguni.

# SHAHADA

Kutoa shahada ni kusema:

أَشْهَدُ أَنْ لَا إِلٰهَ إِلَّا اللّٰهُ وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا رَسُولُ اللّٰهِ

*Ash-hadu an-llaa ilaahailla llahu Wa-ash-hadu-anna Muhammad an- Rasuulullah:*

*“Nashuhudia kuwa hapana Mola ila Allah na Ninashuhudia kuwa Muhammad ni Mtume wa Allah”.*

- Hii ndio shahada, ambayo ndio kiingilio cha Uislamu kutoka kwenye Dini nyingine yoyote.
- Hebu tujiulize, ni kitu gani kilichomo ndani ya matamshi haya kinachomfanya mtu aingie katika Uislamu baada tu ya kuyatamka haya?

- Tukumbuke kuwa maneno haya anaweza kuyatamka mtu yoyote hata kafiri asiye na nia ya kuingia Uislamu.
- Ni dhahiri kuwa kutamka tu haya maneno sio kinachomfanya mtu awe Muislamu bali shahada ya kweli ni ile inayotolewa kwa dhati moyoni, ikadhihirishwa kwa ulimi mbele ya walimwengu na ikathibitishwa kwa vitendo katika utendaji wa kila siku.
- Hivyo, shahada ya kweli ni lazima idhihirike katika sehemu tatu – moyoni, ulimini na matendoni.

# Shahada ya Moyoni

- Ni kawaida ya mtu kutolea ushahidi kile anachokijua vyema.
- Shahidi wa kweli mahakamani ni yule anayeieleza mahakama kama alivyoshuhudia kitendo kikifanyika.
- Hali kadhalika shahada ya kweli inayomuingiza mtu kwenye Uislamu, haina budi kutoka moyoni baada ya kupata ujuzi wa yakini juu ya hao anao washuhudia.

- Kwa maana nyingine kabla ya kutoa shahada, ni lazima kwanza mwenye kushuhudia awe na imani kamili juu ya Allah(s.w) na juu ya Mtume Muhammad(s.a.w).
- Mtume(s.a.w)alitumia muda mrefu wa kipindi cha utume cha Makkah (miaka 13) katika kufundisha imani ili kila mwenye kutoa shahada awe ni mwenye kuitoa kwa dhati moyoni.

- Takriban Masahaba wote waliotoa shahada katika historia, walimpenda Mwenyezi Mungu na Mtume kuliko kitu chochote kile na walikuwa tayari kukabili mateso ya aina yoyote hata kutoa maisha yao kwa ajili ya Mwenyezi Mungu(s.w) na Mtume wake.

- Pia tunajifunza kutokana na historia kuwa wale waliosilimu katika jamii ya Mtume(s.a.w) kwa matamshi tu bila ya kuwa na msukumo kutoka moyoni, waliangukia kwenye unafiki na kuwa maadui wa Allah(s.w) na Mtume wake pamoja na Waislamu.
- Tunafahamishwa juu ya shahada za watu hawa katika aya zifuatazo:

۞ قَالَتِ ٱلْأَعْرَابُ ءَامَنَّا ۖ قُل لَّمْ تُؤْمِنُوا۟ وَلَٰكِن قُولُوٓا۟ أَسْلَمْنَا وَلَمَّا

يَدْخُلِ ٱلْإِيمَٰنُ فِى قُلُوبِكُمْ ۖ............

*”Walisema wanaokaa jangwani; “Tumeamini”. Sema (uwaambie): “Hamjaamini (kweli kweli bado) lakini semeni: “Tumesilimu, (tumesalim amri) maana imani haijaingia vema moyoni mwenu bado”........(49:14).*

# Shahada ya Matamshi

- Japo katika sura ya nje kutamka shahada mbele ya Waislamu huonekana kuwa ndio kibali cha kumuingiza mtu katika Uislamu, kwa kweli hii ni hatua ya pili ya shahada.
- Hatua ya kwanza, ya shahada ni moyoni kama tulivyoona. Lakini kwa nini kutamka shahada mbele ya Muislamu au kikundi cha Waislamu imekuwa ni lazima?

- Kwanini mtu asishuhudie kimoyo moyo tu na akaendelea kuishi kama anavyopaswa aishi Muislamu bila ya kutangazia umma wa kislamu na Walimwengu wote kwa ujumla kuwa naye ni Muislamu?

- Kutamka shahada au kushuhudia mbele ya Muislamu au kundi la Waislamu kumekuwa ni lazima ili kumkaribisha huyu ndugu mpya kwa umma wa Kiislamu.
- Uislamu si Dini ya kimoyo moyo tu ambayo utekelezaji wake huishia kwa mtu binafsi.
- Bali Uislamu ni Dini inayotakiwa isimamishwe katika jamii na iwe juu ya Dini nyingine zote kama Allah(s.w) anavyotufahamisha katika Qur'an:

هُوَ ٱلَّذِىٓ أَرۡسَلَ رَسُولَهُۥ بِٱلۡهُدَىٰ وَدِينِ ٱلۡحَقِّ لِيُظۡهِرَهُۥ عَلَى ٱلدِّينِ

كُلِّهِۦ وَلَوۡ كَرِهَ ٱلۡمُشۡرِكُونَ ﴿٣٣﴾

*"Yeye (Allah) Ndiye aliyemtuma Mtume wake (Nabii Muhammad) kwa uongofu na kwa Dini ya haki ili kuifanya ishinde Dini zote, ijapokuwa makafiri watachukia" (9:33, 61:9).*

هُوَ ٱلَّذِىٓ أَرْسَلَ رَسُولَهُۥ بِٱلْهُدَىٰ وَدِينِ ٱلْحَقِّ لِيُظْهِرَهُۥ عَلَى ٱلدِّينِ
كُلِّهِۦ ۚ وَكَفَىٰ بِٱللَّهِ شَهِيدًا ﴿٢٨﴾

*"Yeye Ndiye aliyemtuma Mtume wake kwa uongofu na Dini iliyo ya haki, ili aishindishe juu ya Dini nyingine zote, Naye anatosha kuwa shahidi" (48:28).*

- Hivyo, ili Uislamu usimame kama Mwenyezi Mungu(s.w) anavyotaka, Waislamu hawana budi kushirikiana bega kwa bega kwa udugu na upendo.
- Na pale Waislamu watakapofanya hivyo ndio wataweza kuusimamisha Uislamu katika jamii.
- Ni kwa msingi huu Allah(s.w) anawaamrisha Waislamu kuishi kidugu na kushirikiana bega kwa bega katika kusimamisha Dini yake.
- Hebu turejee aya zifuatazo:

إِنَّمَا ٱلْمُؤْمِنُونَ إِخْوَةٌ فَأَصْلِحُوا۟ بَيْنَ أَخَوَيْكُمْ ۚ وَٱتَّقُوا۟ ٱللَّهَ لَعَلَّكُمْ
تُرْحَمُونَ ﴿١٠﴾

*“Kwa hakika Waislamu wote ni ndugu; basi patanisheni baina ya ndugu zenu, na mcheni Mwenyezi Mungu ili mpate kurehemewa” (49:10).*

إِنَّ ٱللَّهَ يُحِبُّ ٱلَّذِينَ يُقَٰتِلُونَ فِي سَبِيلِهِۦ صَفّٗا كَأَنَّهُم بُنۡيَٰنٞ مَّرۡصُوصٞ ﴿٤﴾

*“Kwa yakini Mwenyezi Mungu anawapenda wale wanaopigana katika njia yake, safu safu (nguvu moja au mkono mmoja) kama kwamba wao ni jengo lililokamatana barabara” (61:4).*

وَٱعْتَصِمُوا۟ بِحَبْلِ ٱللَّهِ جَمِيعًا وَلَا تَفَرَّقُوا۟ ۚ وَٱذْكُرُوا۟ نِعْمَتَ ٱللَّهِ عَلَيْكُمْ إِذْ
كُنتُمْ أَعْدَآءً فَأَلَّفَ بَيْنَ قُلُوبِكُمْ فَأَصْبَحْتُم بِنِعْمَتِهِۦٓ إِخْوَٰنًا وَكُنتُمْ عَلَىٰ
شَفَا حُفْرَةٍ مِّنَ ٱلنَّارِ فَأَنقَذَكُم مِّنْهَا ۗ كَذَٰلِكَ يُبَيِّنُ ٱللَّهُ لَكُمْ ءَايَٰتِهِۦ لَعَلَّكُمْ
تَهْتَدُونَ ١٠٣

*"Na shikamaneni kwa kamba (Dini) ya Allah nyote wala msifarakane na kumbukeni neema ya Allah iliyo juu yenu, (zamani kabla hamjawa Waislamu) mlikuwa maadui, naye akaziunganisha nyoyo zenu; kwa neema yake mkawa ndugu. Mlikuwa ukingoni mwa shimo la moto, Naye akakuokoeni nalo. Namna hii Allah anakubainishieni aya zake ili mpate kuongoka" (3:103)*

- Aya hizi zinaonyesha jinsi Uislamu usivyoweza kusimama bila ya umoja na udugu miongoni mwa Waumini.
- Hivyo anayeingia katika Uislamu kwa mara ya kwanza ni lazima ajitambulishe kwa Waislamu wenziwe ili washirikiane bega kwa bega katika kuendeleza jamii kwa ujumla.

- Historia ya maisha ya Mtume Muhammad(s.a.w) inatudhihirishia jinsi Uislamu na Waislamu walivyoinukia haraka haraka kutokana na ushirikiano wa kidugu na upendo wa kweli uliojengwa juu ya msingi wa imani thabiti.
- Kwa muda mfupi miaka ishirini na tatu Waislamu waliinukia na kuwa nyota ya ulimwengu.

إِنَّمَا ٱلْمُؤْمِنُونَ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ بِٱللَّهِ وَرَسُولِهِۦ ثُمَّ لَمْ يَرْتَابُوا۟ وَجَٰهَدُوا۟
بِأَمْوَٰلِهِمْ وَأَنفُسِهِمْ فِى سَبِيلِ ٱللَّهِ ۚ أُو۟لَٰٓئِكَ هُمُ ٱلصَّٰدِقُونَ ١٥

*“Wenye kuamini kweli kweli ni wale waliomuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake; kisha wakawa si wenye shaka, na wakaipigania Dini ya Mwenyezi Mungu kwa mali zao na nafsi zao. Hao ndio wenye kuamini kweli’.(49:15)*

- Hivyo shahada ya kweli chimbuko lake ni imani thabiti iliyoshamiri moyoni juu ya kuwepo kwa Mwenyezi Mungu(s.w) na juu ya Utume wa Muhammad(s.a.w).

**(ii) Sunnah**

Mwenendo wa Mtume(s.a.w) na mafundisho yake ndio msingi wa pili wa fiqh. Kila Mtume(s.a.w) alilolifanya na kulielekeza na agizo kutoka kwa Allah(s.a) kamatunavyokumbushwa katika Qur’an.

مَا ضَلَّ صَاحِبُكُمْ وَمَا غَوَىٰ ﴿٢﴾ وَمَا يَنطِقُ عَنِ ٱلْهَوَىٰٓ ﴿٣﴾ إِنْ هُوَ إِلَّا

وَحْىٌ يُوحَىٰ ﴿٤﴾

*“Wala hasemi kwa matamanio(yake). Hayakuwa haya (anayosema) ila ni Wahyi uliofunuliwa (kwake)”(53:2 - 4)*